Kauli Mbadala:
Tunaelekea Wapi?

Mkusanyo wa Safu ya Maoni ya HakiElimu

Kimeharirwa na Rakesh Rajani
Utangulizi na Jenerali Ulimwengu

Wachangiaji: Chambi Chachage, Lilian R. Kallaghe, Aika Kirei,
Richard Lucas, Daniel Luhamo, Agnes Mangweha, James Marenga,
Kajubi Mukajanga, Robert Mihayo, Rose Mushi,
Hebron Mwakagenda, Nyanda Shuli, Gervas Zombwe

Kauli Mbadala:
Tunaelekea Wapi?

Mkusanyo wa Safu ya Maoni ya HakiElimu

Kimeharirwa na Rakesh Rajani
Utangulizi na Jenerali Ulimwengu

Wachangiaji: Chambi Chachage, Lilian R. Kallaghe, Aika Kirei,
Richard Lucas, Daniel Luhamo, Agnes Mangweha, James Marenga,
Kajubi Mukajanga, Robert Mihayo, Rose Mushi,
Hebron Mwakagenda, Nyanda Shuli, Gervas Zombwe

Shukrani
Safu ya *Kauli Mbadala* iliratibiwa mwanzo na Kajubi Mukajanga, aliyeandaa mwongozo na kuchangia uhariri. Michango zaidi ya kiuhariri imetolewa na Robert Mihayo, Nyanda Shuli and Gervas Zombwe. Theophil Makunga, Joster Mwangulumbi na wahariri wa gazeti la *Mwananchi*, wamehakikisha safu hii inawafikia walengwa kila wiki.

© HakiElimu na Mwananchi Communications Limited, 2006 na 2007

HakiElimu, SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (255 22) 2151852/3, Faksi: (255 22) 2152449
www.hakielimu.org • info@hakielimu.org

Mwananchi Communications Limited,
Plot Na. 34/35 Mandela Road,
SLP 19754, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (255 22) 2450878/2450875-6
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

ISBN 9987-423-51-5

Sehemu yeyote katika kitabu hiki inaweza kunakiliwa au kupigwa chapa kwa madhumuni ya kielimu tu na sio biashara. Ili mradi tu shukrani zitolewa kwenye chanzo na nakala mbili zipelekwe HakiElimu na *Mwananchi*.

Yaliyomo

Kuhusu Wachangiaji ii
Utangulizi *Na Jenerali Ulimwengu* iii

Elimu
Serikali ichangamkie tatizo la usafiri wa wanafunzi *Na Kajubi Mukajanga* 1
Tatizo la wanafunzi wanaopata mimba kuahirishwa hadi lini?
Na Kajubi Mukajanga 3
Watoto hawa ni mashujaa *Na Kajubi Mukajanga* 5
Wasomi bado wanahitaji jamii *Na Chambi Chachage* 7
MMEM imeleta mafanikio gani? *Na Aika Kirei* 9
Je kasi ya ujenzi wa madarasa inaathiri ubora? *Na Robert Mihayo* 11
Mitihani ishuhwe daraja machoni mwa serikali na jamii *Na Robert Mihayo* 13
Ruzuku ya MMEM 2006/07: Maswali mengi yanadai majibu *Na Robert Mihayo* 15
Matokeo ya mtihani: Tunafurahia nini hasa? *Na Robert Mihayo* 17
Kulegeza masharti si dawa ya upungufu wa walimu *Na Nyanda Shuli* 19
Je, walimu wetu ni wakombozi? *Na Gervas Zombwe* 21
Mzazi unachangiaje maendeleo ya mtoto? *Na Gervas Zombwe* 23
Wazee vijijini hawajui umuhimu wa kusomesha wasichana? *Na Gervas Zombwe* 25
Elimu tele, lakini malengo yanafikiwa? *Na Gervas Zombwe* 27

Utawala na Uwajibikaji
Mkataba wa KADCO ni kejeli kwa demokrasia? *Na Kajubi Mukajanga* 29
Uongozi ni utumishi, si ubwana *Na Kajubi Mukajanga* 31
Kuwapa taarifa wananchi si hiari, ni lazima *Na Kajubi Mukajanga* 33
Mageuzi polisi jamii yaungwe mkono kwa vitendo! *Na Lilian R. Kallaghe* 35
Rais anahitaji washauri wa aina gani? *Na Rakesh Rajani & Robert Mihayo* 37
Asasi za kiraia zinawajibikaje kifedha? *Na Daniel Luhamo* 39
Muswada wa PCB: Tunapiga hatua au tunarudi nyuma? *By Hebron Mwakagenda* 41
Sera bila utafiti kweli tutafika? *Na Gervas Zombwe* 43
Misitu yetu inamnufaisha nani? *Na Gervas Zombwe* 45
Mfuko wa Majimbo utainufaisha jamii? *Na Rose Mushi* 47
Je kudai uwakilishi 50/50 Bungeni ni sawa? *Na Agnes Mangweha* 49

Afya na Maendeleo
Sheria ya kulinda watoto inamsubiri nani? *Na James Marenga* 51
Tumepata dawa ya foleni za magari? *Na Richard Lucas* 53
Elimu na afya: Upatikanaji kwanza, ubora baadaye? *Na Robert Mihayo* 55
Walemavu: Tatizo ni ulemavu au jamii? *Na Gervas Zombwe* 57

Kuhusu Wachangiaji

Wachangiaji toka HakiElimu

Lilian R. Kallaghe ni Mwandishi wa Habari na alikuwa Meneja Programu ya Habari tangu 2001-2006.

Aika Kirei alikuwa Mchambuzi wa Sera na mtetezi, Idara ya Uchambuzi wa Sera na Utetezi tangu 2005-2007.

Richard Lucas ni Afisa Programu wa Idara ya Upatikanaji Taarifa.

Daniel Luhamo ni Meneja wa Idara ya Fedha na Utawala.

Agnes Mangweha ni mkutubi wa maktaba, Idara ya Upatikanaji Taarifa.

Kajubi Mukajanga alikuwa Mshauri Mkuu, Idara ya Uchambuzi wa Sera na Utetezi tangu 2006.

Robert Mihayo ni Meneja wa Idara ya Upatikanaji wa Habari..

Nyanda Shuli ni Meneja wa Idara ya Habari.

Jenerali Ulimwengu wa Habari Corporation, ni mwandishi na mchambuzi. Pia ni mwanachama na mkurugenzi wa Bodi ya HakiElimu.

Gervas Zombwe ni Mchambuzi wa Sera na Mtetezi, Idara ya Uchambuzi wa Sera na Utetezi.

Wachangiaji toka nje ya HakiElimu

Chambi Chachage ni mtafiti huru na mchambuzi wa masuala ya sera na mashirika ya hiari ya wananchi.

James Marenga ni Meneja wa Programu ya Ushawishi na Habari wa nola.

Rose Mushi ni Mkurugenzi, Action Aid Tanzania.

Hebron Mwakagenda ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la raia la The Leadership Forum ambalo ni mwanachama wa CACI.

Utangulizi

Na Jenerali Ulimwengu

Mara kwa mara, HakiElimu imekuwa ikichapisha matoleo ya makala zinazochokoza mjadala kuhusu masuala muhimu ya maendeleo ya nchi yetu. Kijitabu hiki ni mojawapo ya matoleo hayo na, kama kawaida, kimetokana na kazi nzuri iliyofanywa na watafiti, wanaharakati na wachambuzi mahiri wa masuala ya kijamii, kazi ambayo ilichapishwa kwa mara ya kwanza katika gazeti la Mwananchi chini ya mada, Kauli Mbadala.

Masuala yanayojadiliwa katika kijitabu hiki ni yale yale ambayo yamekuwa yakijadiliwa na wananchi wengi katika majukwaa mbali mbali nchini, ikiwa ni pamoja na ndani ya Bunge, katika makongamano mbali mbali, miongoni mwa wanazuoni na wanaharakati.

Katika upana wake mjadala huu unahusu jinsi ambavyo nchi yetu imebuni mikakati yake ya kimaemaendeleo, na mikakati hiyo, pamoja na utekelezaji wake, vimekuwa na manufaa gani kwa wananchi wa Tanzania. Katika kuyatafakari hayo ni wazi kwamba maswali mengi yanaulizwa, na mara nyingi yanakosa majibu. Lakini ni muhimu kuendelea kuuliza maswali hayo, hadi hapo yatakapopatiwa majibu mwafaka.

Jambo moja linalojitokeza kwa uwazi katika mkusanyiko huu ni kuhusu makuzi na malezi ya watoto wetu, hususan katika nyanja za elimu, afya na usalama wao. Wachangiaji wamesaili aina ya elimu tunayotoa kwa watoto wetu na kujiuliza iwapo kweli elimu hiyo inakidhi mahitaji ya Taifa letu, au iwapo elimu hiyo inawawezesha watoto wetu kujenga uwezo wa kuthubutu kufikiri na kutafuta majawabu kwa maswali wanayokumbana nayo maishani.

Katika muktadha huo waandishi wameuliza iwapo ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kasi kubwa (ambao umefanyika kwa msukumo mkubwa wa Serikali) bila kuandaa waalimu wenye sifa unaweza kutoa elimu bora. Wanauliza iwapo utaratibu wa kuwafundisha waalimu watarajiwa kwa muda wa wiki nne, ili kukabiliana na kasi kubwa ya uandikishaji wa watoto, unafaa katika dunia ya leo, wakati tukipambana na changamoto za utandawazi. Vivyo hivyo kwa mradi wa kujenga zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila tarafa bila kujali maandalizi ya waganga na wauguzi wenye uwezo wa kutoa huduma ya afya kwa viwango vinavyokubalika.

Suala la elimu kwa watoto wa kike limechukua nafasi kubwa katika kijitabu hiki. Kwanza limejadiliwa suala la jumla la umuhimu wa kuwasomesha watoto wa kike, rai ikiwa ni kutaka kutambua manufaa makubwa yanayopatikana kwa Taifa kuwaelimisha wanawake, na umuhimu wa elimu hiyo katika maendeleo ya jamii yo yote.

Lakini pia suala la kuwaachisha shule watoto wa kike wanaopata mimba wakiwa masomoni limejadiliwa, na inabainishwa kwamba mtindo huo haumsaidii yeyote: si wazazi, si jamii na wala si msichana husika. Mapendekezo yametolewa ya namna ya kukabiliana na tatizo hilo ili kuwanusuru watoto hao bila kusababisha madhara yo yote ya kimsingi katika maadili ya uendeshaji wa shughuli ya utoaji wa elimu.

Masuala ya utawala bora yamejadiliwa katika makala kadhaa, kama vile umuhimu wa wananchi au wakilishi wao kupewa taarifa kuhusu mambo yanayowahusu. Mfano umetolewa katika makala moja kuhusu majibu ya waziri Bungeni pale alipotamka kwamba wabunge, ambao ni wawakilishi wa wananchi, hawawezi kupewa taarifa kuhusu mikataba iliyotiwa saini baina ya Serikali na kampuni ya kigeni (KADCO) kwa sababu, kwa mujibu wa waziri, mkataba huo ulikuwa na kipengele kinachozuia taarifa hizo zisitolewe kwa wabunge.

Swali linaloulizwa hapa ni, je iwapo hata wawakilishi wa wananchi (wabunge) hawawezi kupata taarifa hizo, ni nani anazipata, na hiyo mali inayojadiliwa ni mali ya nani hasa? Hili ni suala muhimu katika kipindi hiki mahsusi, wakati bungeni kumezuka mvutano mkubwa kati ya wabunge na Serikali kuhusu usiri unaogubika utiaji wa saini wa mikataba kadhaa. Ni dhahiri kwamba Serikali, kama kweli inajifunza kuhusu uwajibikaji wake kwa wananchi waliyoichagua, basi inajifunza kwa mwendo wa kinyonga.

Suala jingine linahusu hasara linayopata Taifa kutokana na uporaji wa maliasili za misitu yetu, mwandishi akielezea utafiti unaonesha kwamba kiasi cha asilimia 96 ya mapato yanayotakiwa kuingia serikalini yanapotea kutokana na uporaji wa maliasili hizo, kimsingi kwa sababu ya usafirishaji haramu wa magogo na mali nyingine, kutokana na ushiriki wa viongozi wa ngazi za juu serikalini. Utafiti pia umebainisha kwamba wakuu wa serikali wanamiliki hadi asilimia 80 ya makampuni yanayojihusisha na biashara hiyo haramu.

Hiki ni kijitabu muhimu kwa yeyote anayetaka kuelewa na kushiriki katika mjadala wa mikakati ya maendeleo nchini Tanzania, na hii ina maana ya kila Mtanzania anayejali. Nchi hii ni ya Watanzania wote, na wananchi hawana haki ya kuwasabilia wakuu wa serikali jukumu la kuiendesha na kuwaruhusu wafanya watakavyo. Lakini iwapo wananchi wenyewe hawatazinduka na kudai haki ya kushiriki katika utawala wa nchi yao, na kudai taarifa na nyaraka zitakazowawezesha kufanya hivyo, itabidi wajilaumu wenyewe watakapogundua kwamba serikali waliyoiweka madarakani inafanya mambo kinyume cha matarajio yao.

Serikali ichangamkie tatizo la usafiri wa wanafunzi

Na Kajubi Mukajanga
Ilichapishwa 15 Agosti 2006

Kumekuwapo na taarifa nyingi za unyanyasaji wa wanafunzi unaofanywa na wafanyakazi wa daladala, hususan jijini Dar es Salaam. Ama kwa hakika, hakuna mtu yeyote atumiaye usafiri huo ambaye hajashuhudia jinsi watoto wanavyonyanyaswa, na hata kunyanyapaliwa.

Sababu ya hali hii ni kwamba watu wa daladala wanaona kubeba wanafunzi ni hasara. Wanasema wanafunzi ni wengi, na nauli wanayolipa ni ndogo. Kwa hiyo, kubeba wanafunzi kunaweza kusababisha kushindwa kupata mapato yanayohitajika kwa siku.

Wakati huo huo, gharama za mafuta, na uendeshaji kwa ujumla, zimepanda.

Hivi sasa, nauli ya wanafunzi ni shilingi 50 kwa umbali wowote. Nauli halali ya watu wazima ni kati ya shilingi 200 na 300 kutegemea na ruti, japo watu wamekuwa wakilipishwa hadi shilingi 400 (kwa mfano Mwenge – Bunju). Nauli ya shilingi 50 kwa wanafunzi haijabadilika kwa miaka kadhaa sasa, tangu nauli ya daladala ilipokuwa shilingi mia kwa watu wazima.

Sisi tunadhani muda umefika wa kuliangalia jambo hili kwa undani na umakini zaidi. Watoto wetu wanapata shida sana kwenda na kutoka shule. Wanateseka. Lakini je, tumewahi kusikiliza kilio cha hawa watu wa daladala? Tumewahi kujiuliza kama kina mantiki yoyote?

Kwa kawaida, wafanyakazi wa daladala hupewa kiwango maalum cha pesa wanazopaswa kulipa kwa siku, yaani hesabu. Ni jukumu la dereva na kondakta kuhakikisha hesabu inapatikana. Mwenye gari hawezi kukubali kuambiwa mapato yameshuka kwa kuwa wamepakia wanafunzi wengi siku hiyo. Yeye atauliza: wazazi wananichangia gari linapokwenda gereji?

Na hicho ndicho kiini cha tatizo. Ikiwa Serikali haitoi ruzuku kwa wenye magari, kwa nini wenye magari watarajiwe kuubeba mzigo huu peke yao?

Hakuna biashara nyingine ambayo wafanya biashara wanalazimishwa kutoa nafuu kwa huduma za wanafunzi. Ukienda kununua nguo, umeme, maji, au hata chakula hakuna bei ya mwanafunzi na mtu mzima. Huwezi kudai punguzo kwa kuwa nyumbani kwako kuna wanafunzi kadhaa wanaokutegemea. Wala mwenye gari hawezi kudai nafuu anaponunua mafuta au vipuri kwa kuwa anabeba wanafunzi.

Hata hivyo, lazima tuelewe kuwa hapa kuna tofauti ya msingi. Tunaongelea suala la kuhakikisha watoto wetu wanahudhuria shuleni. Ni suala la kuelimisha taifa. Kwa hiyo lazima tunoe bongo, tutafute njia ya kuhakikisha hilo linafanyika bila kuwategemea wenye daladala binafsi pekee.

Tufanyeje? Sisi tunadhani kuna haja ya kuanzisha mjadala wa wadau ili kutafuta ufumbuzi endelevu, ambapo mapendekezo mbalimbali yatajadiliwa.

Wakati watu wazima wakilipa shilingi mia, wanafunzi walikuwa wakilipa nusu ya nauli. Katika nchi nyingi ambazo kuna utaratibu wa kutoa nafuu kwa wanafunzi, wanafunzi hulipa nusu. Je, na sisi turejee huko, ili

mzigo usiwaelemee wenye magari peke yao, na tuweze kuwapunguzia vijana wetu adha?

Je, inawezekana kuteua idadi fulani ya magari katika kila ruti ili yabebe idadi fulani ya wanafunzi kila tripu na kuyapa ruzuku au nafuu maalum?

Chama cha wenye mabasi ya daladala jijini Dar es Salaam (DARCOBOA) inasemekana kilikubali utaratibu ambapo mabasi makubwa, yaani DCM na Coaster, yangebeba wanafunzi 10 na madogo, "vipanya", wanafunzi wanne. Utaratibu huu ungepunguza adha ya watoto. Hata hivyo, hili halifanyiki. Askari, ambao walipaswa kusimamia utaratibu huu, hawafanyi hivyo, hata wanapokuwa katika vituo vya mabasi.

Tatizo la askari kutosimamia utaratibu huu linaweza kusababishwa na ukweli kwamba wao wenyewe, japo wanalipwa mishahara, wanapanda daladala bure. Ni vigumu kumkemea mtu anayekupa huduma bure wakati unalipwa mshahara na yeye hapati ruzuku kwa kukuchukua bure!

Uongozi wa DARCOBOA unasisitiza kuwa utaratibu huo bado upo. Zichukuliwe hatua gani kuhakikisha unafuatwa na hata kuboreshwa?

Muda umefika wa suala hili kutafutiwa ufumbuzi wa kitaifa. Ni suala la kuwawezesha watoto kupata elimu, hivyo si suala la mzazi binafsi au DARCOBOA. Serikali inawajibika kutoa uongozi na kudhamiria kupata ufumbuzi. Waziri Mkuu amesema elimu ni kipaumbele cha kwanza kwa serikali ya awamu ya nne. Jambo hili pia linahusu elimu. Litashughulikiwaje?

Tatizo la wanafunzi wanaopata mimba kuahirishwa hadi lini?

Na Kajubi Mukajanga
Ilichapishwa 22 Agosti 2006

Hivi karibuni mjadala uliibuka upya kuhusu tatizo la mimba shuleni, na hasa kitu gani kifanyike kuhusu watoto wanaopata mimba. Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ilitoa msimamo wake Bungeni kwamba sera hairuhusu wanafunzi wanaopata mimba kuendelea na masomo katika mfumo rasmi wa kawaida.

Lakini baadae, ikiwasilisha mapendekezo yake kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii iliitaka Serikali kufuta kanuni inayotumika kuwafukuza shule watoto wanaopata mimba. Kamati ilisema utaratibu huu si mzuri na hakuna anayenufaika nao.

Kwa mujibu wa taarifa za gazeti la *The Guardian*, takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2001 na 2005 wasichana 12,413 walilazimika kuacha shule kutokana na ujauzito. Hata hivyo, ukweli ni kwamba siyo rahisi kupata takwimu sahihi, kwani kuna wengi wanaoacha shule kutokana na uja uzito lakini kumbukumbu rasmi huonyesha tu kwamba watoto hao ni "watoro". Hii ni kutokana na aibu na unyanyapaa unaoandamana na kupata mimba shuleni, na wasichana wengi wamekuwa wakijiondoa kimya kimya. Bila shaka idadi kamili ni kubwa zaidi kuliko takwimu rasmi.

Kufukuzwa shule kwa ujauzito kunaweza kuwa moja ya sababu za idadi ya wanaume na wanawake kutofautina mno katika vyuo vya elimu ya juu nchini.

Kwa kweli suala la majaaliwa ya watoto wanaopata mimba shuleni lazima sasa lijadiliwe kwa uwazi ili itayarishwe sera itakayozingatia ukweli wa hali halisi.

Sababu kubwa inayotolewa na watetezi wa mfumo uliopo hivi sasa ni kuwa kwanza ni makosa kwa watoto kujihusisha na ngono wawapo shuleni, na kosa hilo lazima litolewe adhabu.

Wanaendelea kueleza kwamba kuruhusu wasichana wanaopata ujauzito kuendelea na masomo, hata baada ya kujifungua, kuna hatari ya kulea tabia mbaya shuleni, ambapo watoto wataendekeza ngono kuliko kilichowapeleka shuleni, yaani masomo.

Wanauliza pia jinsi gani msichana mwenye mimba au mwenye mtoto ataweza kuwa makini darasani huku akiwa na afya legelege ya ujauzito au majukumu ya umama.

Hayo ni maangalizo na hofu za msingi. Hata hivyo, ni muhimu kuliangalia suala hili kwa undani na mapana zaidi. Ni muhimu uongozi wetu uwe na ujasiri wa kuikabili changamoto iliyopo bila kuukwepa ukweli kwamba kwa miaka nenda rudi, tumekuwa tukiwahubiria binti zetu kuepuka ngono na tukiwaachisha masomo wanapopata mimba lakini tatizo limebaki pale pale.

Kwanza, kama ilivyosema Kamati ya Bunge, tujiulize, nani amewahi kufaidika na adhabu hii? Si mtoto aliyepata mimba, si wazazi, wala si taifa. Wote wanakuwa wamepoteza. Lakini mbaya zaidi, anakuwa

ameadhibiwa hata mtoto ambaye hajazaliwa, kwani sote tunajua kuwa kumzuia mama yake kupata elimu ni kuathiri pia maisha na makuzi ya mtoto atakayezaliwa.

Ufumbuzi wa tatizo hili una sehemu tatu muhimu. Kwanza, tuwajengee watoto wa kike mazingira yatakayosaidia kuwaondoa katika hali ya kujikuta wamelazimika kuingia katika ngono, sambamba na kuinua hadhi ya mtoto wa kike katika jamii. Tunaelewa kwamba zipo mimba zinazotokana na kubakwa, kudanganywa, au hata tamaa ya mwili wakati wa balehe na ujana. Tuwasaidie binti zetu kuweza kupembua mambo na kufanya maamuzi sahihi, lakini pia tuwajengee kujiamini.

Pili, kwa kuwa wapo ambao bado watafanya ngono licha ya mahubiri na makatazo yote, basi tutoe elimu kwa vijana wetu itakayowasaidia kuepuka mimba na magonjwa ya ngono kama UKIMWI na mengineyo.

Na tatu, tuweke utaratibu wa kuwasaidia wale walioanguka kabisa na kujikuta wakiwa waja wazito, badala ya kuwatupilia mbali. Na utaratibu huu si mwingine bali ule utakaowawezesha kukamilisha elimu yao. Elimu itawasaidia kwanza kuepuka mimba nyingine zisizotarajiwa siku za usoni, lakini pia elimu itawasaidia kupata stadi za kujikimu wenyewe na watoto wao.

Na jambo hili linawezekana. Kenya, kwa mfano, wana Sera ya Jinsia na Elimu ya mwaka 2003 ambayo inatoa mwanya kwa wasichana waliopata ujauzito wakiwa shuleni kurejea na kukamilisha masomo yao, na hata kwenda katika shule nyingine ili kuondokana na unyanyapaa unaoweza kuwakuta ikiwa watarudi katika shule zao za awali.

Msumbiji wasichana huruhusiwa kuendelea na masomo yao baada ya kujifugua na hutakiwa kusoma shifti za jioni. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kwamba utaratibu huu wa kusoma jioni hautiliwi maanani sana na kuna wanaosoma asubuhi.(Helgesson, L, *Getting Ready for Life: Life Strategies of Town Youth in Mozambique and Tanzania*, uk.159.)

Ingekuwa vizuri Watanzania wakakubali kwamba jukumu la jamii na serikali ni kujitahidi kuwapa elimu watoto wote, wakiwamo waliopata mimba. Mara nyingi katika jamii zetu sheria ya kuwapatiliza wanafunzi wanaopata mimba imekuwa ikiwaathiri zaidi watoto wa maskini. Watoto wa tajiri na wa viongozi wamekuwa wakihamishwa shule au kupelekwa nje ya nchi na kuendelea na elimu.

Wapo wanawake ambao walipata mimba walipokuwa shuleni, wakafukuzwa, lakini baadae wakahangaika wenyewe wakajisomesha na sasa wanatunza familia zao. Kuna haja ya sauti za wanawake hawa kusikilizwa na viongozi. Hali kadhalika kuna wanataaluma ya elimu na wanasaikolojia ambao nao wanaweza kutoa mawazo kuhusu tatizo hili. Tusikilize pia sauti za watoto wanyonge waliokatishwa masomo kwa mimba. Kwa kifupi, viongozi wetu wakubali kupokea maoni anuwai ili kukabiliana na tatizo hili

.

Watoto hawa ni mashujaa

Na Kajubi Mukajanga
Ilichapishwa 29 Agosti 2006

Mfumo wa malezi na elimu yetu unasisitiza kumfunza mtoto utiifu na adabu. Mtoto anatakiwa awasikilize wakubwa wake, wakiwamo wazazi, walimu na wakubwa wengine katika jamii. Dhana ni kwamba wakubwa watawafunza watoto mambo mazuri na muhimu katika maisha, na watoto wanapaswa kujifunza toka kwa wakubwa.

Kwa ujumla, dhana hii haina tatizo, na imeongoza makuzi na malezi ya jamii zetu kwa vizazi nenda rudi. Lakini je, pale ambapo jamii inakaa kimya wakati watoto wanapomaizi tatizo na kutaka litatuliwe, watoto wafanyeje?

Maana ni muhimu kukumbushana kwamba kuwa mdogo hakumwondolei mtoto haki na uwezo wa kufikiri, kutamani, kuota ndoto, kudhamiria. Na makuzi na elimu nzuri ni ile itakayochochea udadisi katika mtoto, itakayomwezesha kutafakari na kuchambua, itakayomsukuma kuusaka ukweli badala ya kuwa kasuku.

Makuzi na elimu nzuri, kama alivyowahi kusema mwanafalsafa Issa Shivji, ni ile itakayomwezesha mtoto "kuthubutu kufikiri, na kufikiria kuthubutu".

Na leo basi tuongelee tukio moja la kusikitisha lakini ambalo limetoa funzo kubwa katika muktadha huu.

Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari vikinukuu vyanzo vya kipolisi, mnamo tarehe 15 Agosti mwaka huu, saa 11.00 jioni katika Barabara ya Kawawa, Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mtoto wa miaka mitano aligongwa na gari na kufariki. Marehemu Fahad Ayubu alikuwa akisoma chekechekea katika Shule ya Mtambani na mauti yalimkuta akitokea shuleni kuelekea nyumbani.

Habari zinaeleza kuwa kwa muda mrefu, wanafunzi wa shule hiyo, pamoja na uongozi wa shule, wamekuwa wakilalamikia mwendo wa kasi wa magari na wakiomba matuta yajengwe katika eneo hilo ili kuwalazimisha madereva kupunguza mwendo na hivyo kuepusha uwezekano wa janga kama hilo.

Inaelekea kwamba maoni na maombi hayo yalipuuzwa na mamlaka husika.

Vyombo vya habari vimenukuu barua zilizoandikwa na uongozi wa shule tangu mwaka 2003 kwenda Manispaa ya Kinondoni baada ya mwanafunzi mwingine wa shule hiyo kugongwa.

Baada ya shinikizo la muda mrefu, vyombo vya habari vinasema Aprili 22 mwaka huu, Mkuu wa Polisi Usalama Barabarani aliandika barua kumtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kuzingatia ushauri wa uongozi wa shule. Barua hiyo, iliyoandikwa na Mrakibu Msaidizi Amir Kinja kwa niaba ya Mkuu wa Usalama Barabarani, haikuwa imezingatiwa hadi siku mtoto Fahad alipogongwa na kufa papo hapo.

Vyombo vya habari vimewanukuu walimu wa Mtambani wakieleza kwamba kuna mwanafunzi mwingine wa Chuo Kikuu cha Tumaini kilicho jirani na eneo hilo, kwamba naye aligongwa na gari na kufa.

Kama hiyo haitoshi, miaka kadha iliyopita mwanafunzi wa Seminari ya Kiislamu ya Mkwajuni, iliyo umbali wa takriban nusu kilomita toka Mtambani katika barabara hiyo hiyo, aligongwa na kufa, na ndipo mamlaka zikajenga matuta katika eneo hilo la Mkwajuni.

Inaeleweka basi kwa nini kifo cha Fahad Ayubu siyo tu kiliwasononesha watoto wenzie, bali kiliwaudhi mno. Siku iliyofuata, wanafunzi wa Mtambani waliamua kufunga Barabara ya Kawawa katika eneo hilo kudai wasikilizwe.

Wanafunzi walikuwa wakipinga kile walichokiona kuwa ni jeuri na kutojali kwa Manispaa, iliyogoma kuweka matuta, hali waliyoona kuwa ndiyo iliyosababisha kifo cha mwenzao mdogo.

Wanafunzi walikuwa wakiimba "tunataka matuta" huku wakiishutumu Manispaa. Waliifunga barabara kwa umati wao, na kwa kulala barabarani, hadi askari walipokuja.

Tukio hili linasikitisha, lakini linatupatia mafunzo mawili muhimu.

Kwanza, tujifunze kwasikiliza watoto wetu. Dhana ya kwamba mtoto ni mtoto tu na hana ajualo ni dhana ya kikale isiyoweza kuthibitishwa kisayansi wala kitaaluma. Ni lazima tuwatilie maanani watoto pale wanapoongelea masuala yanayowahusu. Ikiwa ni kuwasaidia na kuwaongoza, tutafanyaje hivyo ikiwa hatusikilizi hata wanachosema?

Pili, kwa kuwa kitendo cha watoto kiliufanya umma na baadhi ya mamlaka, kama vile ya usalama barabarani, kabaini tatizo hilo, ni wazi basi kwamba ni muhimu kuwapa malezi na elimu ambayo itasaidia kuwafanya waongee, wapaaze sauti, wathubutu. Tuwape makuzi na elimu ambayo wakati ikisisitiza adabu, isiwageuze watoto kuwa ma-'hewala bwana' bila kutafakari.

Watoto wa Mtambani wametoa hoja yao. Wamethubutu kulala barabarani kumlilia mwenzao na kuzilazimisha mamlaka kuwasikiliza. Wamekataa ukondoo. Hiki ni kizazi kipya kinachotaka kusikilizwa. Kinachothubutu. Watoto hawa ni mashujaa wa kweli.

Je, kuna kiongozi mwenye ujasiri wa kuwapongeza vijana hawa wadogo na kutamka hadharani kwamba tumejifunza kutoka kwao?

Wasomi bado wanahitaji jamii

Na Chambi Chachage
Ilichapishwa 31 Oktoba 2006

Jumamosi, Oktoba 14, tuliadhimisha siku ya kumbukumbu ya aliyekuwa Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere. Hii ni siku ambayo Mwalimu Nyerere alifariki dunia miaka saba iliyopita. Kama ilivyo ada, maadhimisho hayo yalitoa fursa kwa jamii kujifunza na kutafakari kuhusu maisha na fikra za Mwalimu. Tuliweza kusoma au kusikiliza hotuba zake kwenye vyombo vya habari. Tupo tuliobahatika pia kupata nakala za vitabu vyake.

Je, siku hii imetuachia kumbukumbu gani ya msingi itakayotusaidia kujenga jamii yetu? Imetuongezea hamasa gani katika mapambano yetu dhidi ya wale maadui watatu wa maendeleo aliowaainisha Mwalimu Nyerere, yaani ujinga, umaskini na maradhi? Je, sisi kama viongozi, wasomi, wataalamu au wananchi wa kawaida tumejifunza nini kutoka kwa Mwalimu? Je, tunaendelea kutafakari na kujifunza kutoka kwa Mwalimu kila siku au tunasubiri mpaka Oktoba 14, 2007? Na siku hiyo itakapofika tutakuwa tumepiga hatua gani katika kuyaendeleza yale aliyojitahidi kuyaendeleza Mwalimu?

Jambo mojawapo ambalo Mwalimu alipenda kutusisitizia sana ni kuhusu uhusiano kati ya elimu na jamii. Na hii haimaanisha uhusiano kati ya elimu na jamii tu, bali pia inamaanisha uhusiano kati ya wenye elimu na jamii yao. Elimu inayotolewa na jamii, alisisitiza Mwalimu, haina budi kuwa na manufaa kwa jamii hiyo. Kwa mtazamo wa Mwalimu, kazi kubwa ya elimu ilikuwa ni kumwezesha mtu kupambana na mazingira yanayomzuia yeye na jamii yake kustawi. Hivyo, alisisitiza kuwa elimu yetu haina budi kutuandaa kwanza kwa maisha na haja za Tanzania.

Mtu aliyepata elimu, yaani msomi, mtaalamu au mhitimu, anahitaji jamii na anawajibika kwayo. Jamii nayo inahitaji watu walio na elimu na inawajibika kuwapatia elimu hiyo. Mwalimu hakutaka kuona jamii yetu ikitoa elimu ambayo inajenga na kutenganisha matabaka ya waliosoma na wasiosoma. Elimu aliyojaribu kuijenga Mwalimu ni ile inayohakikisha kwamba waliosoma wanajitambua kwamba ni sehemu ya jami, na kwa kuwa wamepata nafasi zaidi kuliko wasiosoma, basi wajibu wao kwa jamii ni mkubwa zaidi.

Kuna umuhimu wa kuwa na mjadala wa kitaifa kuhusu mtazamo huu wa Mwalimu. Umuhimu huu unatokana na ukweli kuwa jamii bado ndio inayogharimia kwa kiasi kikubwa elimu inayotolewa nchini. Wananchi wanachangia ujenzi wa madarasa. Wanajitolea kujenga nyumba za walimu. Na zaidi ya yote, wananchi wanalipa kodi. Je, ni kwa kiasi gani wananchi wanayafaidi matunda ya mchango wao katika kutuelimisha? Je, wanashiriki na kushirikishwa vipi katika mipango ya maendeleo ya elimu? Je, watu waliosomeshwa na jamii wanashirikiana vipi kwa ukaribu na jamii yao katika kupambana na umaskini, maradhi na ujinga?

Katika hotuba yake ya *Msomi Anahitaji Jamii*, Mwalimu Nyerere alisisitiza kuwa:"Maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana bila wananchi wenyewe kushiriki. Watu wenye elimu wanaweza kujitokeza kuongoza, na wanapaswa kufanya hivyo. Wanaweza wakaonesha

mambo yanayowezekana kufanywa, na jinsi yanavyoweza kufanyika. Lakini wanaweza tu kufanikiwa kuleta mapinduzi kwa watu kama watafanya kazi zao pamoja na wananchi. Ndio kusema kwamba, watu wenye elimu wanaweza tu kuwa na faida kama watachanganyika kabisa na kuwa sehemu ya jamii wanayotaka kuisaidia." Je, tunafanya hivyo?

Je, wasomi wetu wa vyuo vikuu, vyuo vya ufundi na vyuo vya ualimu wanafanya kazi pamoja na wananchi? Je, wataalamu wetu wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) wanachanganyika na wananchi? Je, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) unawaandaa wanafunzi kuwa na faida kwa jamii inayowazunguka? Je Mpango wa Elimu ya Msingi kwa wale Walioikosa (MEMKWA) unawaandaa vijana kwa maisha na haja za Tanzania?

Itakuwa vyema kama tutaipitia upya sera ya *Elimu ya Kujitegemea* aliyoitoa Mwalimu Nyerere mwaka 1967. Kwa wasomi wa leo, pengine sera hiyo itaoenakana imepitwa na wakati katika zama hizi za utandawazi. Lakini kama Mwalimu alivyotuasa miaka miwili kabla ya kifo chake, bado kuna mengi ya kujifunza kutokana na kutekelezwa au kutotekelezwa kwa sera hiyo. Jambo mojawapo la kujifunza ni namna ya kuzifanya shule za msingi ziweze kutoa elimu inayotutosheleza kwa kushirikiana na jamii. Hatuna budi kulizingatia hili katika mipango yetu ya elimu kwa kuwa shule hizi ndio zinajenga msingi wa uhusiano kati ya msomi na jamii.

Njia mojawapo inayoweza kutumika kuimarisha msingi huu ni kwa kuwawezesha wanafunzi wawe na ziara za mafunzo katika vijiji, vitongoji na mitaa yao. Hii itatawawezesha kuchangamana na wananchi na kujifunza jinsi wanavyoendesha maisha yao. Kwa mfano, darasa la sayansi linaweza kujifunza jinsi fundi seremala anavyotumia nyenzo za madaraja mbalimbali katika shughuli zake; darasa la sanaa linaweza kujifunza jinsi vyungu au vikapu vinayotengenezwa; na darasa la lugha linaweza kujionea jinsi kitabu kinavyohaririwa na kuchapishwa.

Shule pia zinaweza kutumia siku maalumu ya kujumuika shuleni, maarufu kama *Open Day*, kuendesha midahalo inayojumuisha wananchi na wanafunzi. Midahalo hii inaweza kuzungumzia masuala mbalimbali ya maendeleo ya shule na jamii kwa ujumla. Pale inapowezekana, wananchi na wanafunzi wanaweza kushirikiana kufanya kazi mbalimbali zinazoendana na mitaala, umri na uwezo wa wanafunzi.

Hakika mawazo ya Mwalimu Nyerere kuhusu uhusiano kati ya elimu na jamii yanaibua maswali mengi kuhusu azma yetu ya kujenga taifa lililoelimika. Hatuna budi kuyatafakari maswali haya kwa kina hasa katika kipindi hiki ambacho jamii yetu inahitaji mipango endelevu ya maendeleo. Na wasomi wetu wanaweza tu kuyapata majibu ya dhati ya maswali haya kutoka kwenye jamii inayowazunguka. Jamii ndio kioo na kipimo cha usomi. Kama hotuba ya Mwalimu Nyerere inavyotukumbusha, wasomi bado wanahitaji jamii na jamii bado inawahitaji wasomi.

MMEM imeleta mafanikio gani?

Na Aika Kirei
Ilichapishwa 16 Januari 2007

Awamu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) imeisha rasmi mwishoni mwa mwaka 2006. Awamu ya pili imeanza mwaka huu na itaendelea hadi mwisho wa mwaka 2011. Je, tunafahamu mafanikio ya awamu ya kwanza? Mapungufu yake? Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji?

Haya ni baadhi ya maswali ambayo watunga sera na watekelezaji inawabidi kuyafikiria. Japokuwa tathmini za mpango wa kwanza wa MMEM zimekuwa zikifanyika kila mwaka, kilichomuhimu ni kutumia mafunzo hayo katika sera na utekelezaji wa awamu ya pili. Je, imefanyika?

MMEM inalenga kupanua uandikishaji, kuinua ubora wa elimu, na kuboresha usimamizi wa mfumo mzima wa elimu.

Uandikishaji
Ifikapo 2006, mpango huu ulilenga kuandikisha jumla ya wanafunzi 6,847,692 katika darasa la kwanza. Kutokana na ripoti ya mwisho ya kutathmini utekelezaji mzima wa MMEM, ilibainika kuwa jumla ya wanafunzi 7,146,974 waliandikishwa. Haya kweli ni mafanikio makubwa yanayostahili kusifiwa.

Hata hivyo, uandikishaji sio sawa na kusoma. Je, tunafahamu wanafunzi wangapi walihudhuria baada ya kuandikishwa? Je ni asilimia 95%? 85%? 70%? Hatuna uhakika, kwa sababu takwimu hizi hazipatikani katika ngazi ya taifa. Ila, wanaopita mashuleni mara nyingi hushangaa kuona asilimia kubwa ya wale walioandikishwa hawapo madarasani.

Pamoja na sababu nyinginezo, kutokuwepo kwa walimu wa kutosha, na walimu kutohudhuria shuleni wakishughulikia mambo mbalimbali inachangia tatizo hili.

Lengo lilikuwa kuajiri walimu 45,798 wapya ifikapo mwisho wa mwaka 2006. Serikali ilifanikiwa kuajiri jumla ya walimu wapya 50,991. Haya ni mafinikio makubwa. Baada ya kuwaajiri, walimu wanahitaji mazingira yatakayowawezesha kufundisha vizuri. Tathmini imeonyesha kuwa motisha ya kuwafanya walimu, wengi wao wakiwa ni vijana, kubaki vijiji walivyopangiwa ni hafifu. Nyumba nyingi za walimu ni za udongo na zinakaribia kuporomoka. Mishahara yao ni midogo wakati majukumu ni mengi, vifaa vya kufundishia ni haba, na uandaaji wa walimu hao kukabiliana na hayo yote hautoshi.

Ubora wa elimu
Walimu ni kiini cha elimu. Serikali ililenga kuboresha uwezo wa walimu kufundisha na kutoa ruzuku maalum (Capitation Grant) ya dola za Kimarekani kumi (au Shilingi 12,500/-) kwa kila mwanafunzi kununua vitabu na vifaa vingine vya kujifunza.

Lakini, pamoja na elimu kupata bajeti kubwa kuliko sekta nyingine yoyote, ripoti ya utekelezaji wa MMEM imebaini kuwa upungufu wa fedha ulizuia walimu 68,289 waliopangwa katika kipindi chote cha MMEM kupata mafunzo ya kazini.

Mwalimu Nyerere alishawahi kutukumbusha kwamba walimu ni muhimu zaidi kuliko hata viongozi wakubwa, kwa sababu wanaandaa kizazi kipya. Mafanikio na maendeleo ya nchi yetu yako mikononi mwa walimu wetu. Katika karne ya 21,

haitoshi kufundisha kwa kuandika na chaki ubaoni. Tunahitaji mbinu za kisasa, mbinu shirikishi, zitakazomwezesha mwanafunzi kufikiri tofauti na ilivyo kawaida, kuuliza maswali, kuchambua na kutathmini, kuwa mbunifu na kutunga mambo mapya, kujiamini na kuwa mjasiri. Uwezo wa aina hii ndiyo utatuwezesha kuijenga nchi, kutatua matatizo, na kutengeneza ajira. Elimu ni uwezo, sio tu uandikishaji au cheti. Je, walimu wetu wanapewa mwongozo na mazingira ya kuendeleza uwezo wao?

Usimamiaji wa mfumo wa elimu
Utawala na usimamiaji bora wa mfumo wetu mzima wa elimu ni uti wa mgongo wa mafanikio. Fedha za MMEM zilikusudia kujenga madarasa ya wanafunzi ili wasiendelee kukaa chini ya mwembe, kuwajengea walimu nyumba ili wasiendelee kulala kwenye sakafu ya udongo, na kuwaongezea walimu vifaa vya kufundishia na wanafunzi vifaa vya kujifunzia.

MMEM imekaguliwa mara kwa mara na wakaguzi mbalimbali (kama Deloitte & Touche, KPMG) lakini kwa bahati mbaya ripoti hizi hazijawekwa hadharani. Hata hivyo, bado tunasoma magazetini karibu kila siku habari za ubadhirifu wa fedha za MMEM (na pia MMES). Matumizi mabaya ya fedha yanawanyima watoto wetu haki yao ya kupata elimu. Je, wahusika wanawajibishwa? Mfumo unarekebishwa kuhakikisha fedha zitatumika vizuri zaidi? Pengine kuandaa na kuweka hadharani ripoti kamili za wakaguzi na hatua thabiti zilizochukuliwa na Serikali ingesaidia.

Ripoti ya awali iliyofanywa na REPOA kwa niaba ya Wizara ya Fedha (PETS) ilionesha kuwa asilimia kubwa ya ruzuku ya "capitation" haikufika shuleni kwa muda uliopangwa. Ripoti hii ilitoa mapendekezo ya kufanya fedha hizi ziwafikie walengwa kwa muda. Ni vigumu kuelewa kama mapendekezo haya yamefanyiwa kazi au la. Pengine kurudia zoezi la PETS na kuthibitisha hali halisi ya sasa hivi ingesaidia.

Kwa ujumla, MMEM imeleta mafanikio mengi, muhimu na makubwa katika elimu ya msingi. Kwa kuondoa ada, imeweza kupanua upatikanaji wa elimu kwa watoto wengi ambao kabla ya hapo, wazazi wao wasingekuwa na uwezo wa kuwapeleka shuleni. Lakini, baada ya kushinda pambano hilo, sasa tusisitize mafunzo. Tusiridhike tu kuwa wanafunzi wengi wameandikishwa na madarasa mengi yamejengwa. Badala yake tuhakikishe kuwa elimu wanayoipata madarasani itawawezesha kumudu maisha. Elimu ni kujifunza, siyo madarasa tu. Elimu ni uwezo, siyo cheti.

Je kasi ya ujenzi wa madarasa inaathiri ubora?

Na Robert Mihayo
Ilichapishwa 23 Januari 2007

Hivi karibuni kulikuwa na taarifa kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilielezea wasiwasi wake kuhusu ubora wa madarasa yaliyokwishajengwa na yanayoendelea kujengwa katika mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMES). Juzi tumesikia hata Waziri Mkuu Edward Lowassa akiunda kamati ya kuchunguza ubora wa majengo ya sekondari kote nchini.

Kwa siku za hivi karibuni tumesoma taarifa Waziri Mkuu na viongozi wengine wa juu wakihimiza ujenzi wa madarasa ya kutosha ili kuhakikisha angalau asilimia 75 ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu katika kila wilaya nchini wanapata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari pia amesisitiza kuzingatia ubora wa madarasa hayo yanayojengwa.

Kwa mujibu wa taarifa hizi, Waziri Mkuu amewapa changamoto viongozi wa kila mkoa na wilaya nchini kuhakikisha kuwa ifikapo Machi 15 mwaka huu, madarasa haya yawe tayari kwa watoto kuanza masomo yao ya sekondari.

Kamati ya Bunge, Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla wanastahili pongezi kwa kulivalia njuga suala hili la ubora wa majengo ya madarasa. Inaonesha uchungu walionao katika kuhakikisha kuwa walimu na watoto wetu wanatendewa haki. Hata hivyo ningependa kuainisha machache tu.

Kwanza, majengo ya madarasa yakiwa dhaifu ni mzigo kwa taifa kwa vile kila mara yatahitaji fedha kwa ajili ya ukarabati au hata ujenzi mpya badala ya fedha hiyo kutumika katika ujenzi wa madarasa mapya.

Lakini pili ni ukweli usiopingika pia kuwa madarasa duni ni hatari si kwa maisha ya wanafunzi lakini pia kwa walimu kwani yanaweza kuporomoka na kuleta maafa wakati wowote.

Aidha, ni dhahiri pia kuwa fedha inayotolewa na serikali lazima itumike kwa kiwango na ubora wa kazi iliyotarajiwa,. Kinyume cha hapo itakuwa ni kuwaibia walipa kodi.

Lakini hapa inabidi Kamati ya Bunge na wananchi wote tujiulize: hivi ni kwa nini hasa tatizo hili limekithiri kwa sasa wakati hapo awali halikuwapo? Kwa nini madarasa hafifu yanaendelea kujengwa?

Mimi ninavyoelewa ni kuwa Wizara ya Elimu ina viwango vya ubora wa madarasa, yawe ya shule za msingi au za sekondari. Sasa inakuwaje viwango hivi havizingatiwi?

Je, inawezekana pengine viwango hivi havijapelekwa shuleni na hivyo havifahamiki kwa wadau wakiwamo mainjinia wa ujenzi wa wilaya, walimu, halmashauri za wilaya na kamati za shule?

Je, inawezekana pengine ingawa viwango hivi vimesambazwa kunakohusika lakini kwa sababu mbalimbali za msingi au hata kwa makusudi tu wanaopaswa kuvitumia hawafanyi hivyo?

Je, inawezekana pengine wanaopaswa kuvitumia viwango hivyo licha ya kuwa na nia ya kuvitumia viwango hivyo pengine wanakwamishwa na sababu ambazo bado

hazijahamika zikiwemo za rushwa na ubadhirifu?

Je, inawezekana pengine kiasi cha pesa zinazotolewa kwa ujenzi wa madarasa yanayolingana na viwango vinavyotakiwa ni pungufu kukidhi lengo hilo?

Kwa mujibu wa MMEM kila darasa limetengewa dola za Kimarekani 4,000 (takribani shilingi milioni 5). Lakini badala yake bajeti na ruzuku inayopelekwa ni shilling milioni 3.1 tu kwa kila darasa la shule ya msingi. Pesa hizi zinatosha kufikia viwango?

Kama hilo halitoshi kuna madai kuwa katika baadhi ya sehemu za Tanzania pengine katika hamasa ya kuongeza idadi ya madarasa katika maeneo yao, baadhi ya viongozi huwalazimisha wananchi wajenge madarasa hata mawili kwa pesa hiyo hiyo. Je, maelekezo hayo yanaweza kusababisha madarasa hayo kutofikia viwango?

Kwa hiyo wakati tunaipongeza Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Waziri Mkuu, pamoja wa viongozi wengine kwa kuhimiza na kusimamia kidete ujenzi wa madarasa, kuna haja pia ya kuhakikisha kuwa kasi hii ya ujenzi sharti iendane na ubora wa madarasa hayo.

Ninachotaka kusema ni kuwa lazima kuwe na uwiano kati ya kasi ya ujenzi wa madarasa na ubora wa madarasa hayo; achilia mbali ubora wa elimu itolewayo katika shule hizo. Kasi mpya bila ubora haitatupeleka tunapohitaji kufika.

Kuna haja kwa Wizara za Elimu na ile ya serikali za Mitaa kuweka bayana viwango vya ubora wa madarasa; kuanzia ya msingi hadi za sekondari, hata kwa kupitia magazetini. Pia kuna haja ya kuhakikisha kuwa viwango hivyo vimeandikwa katika lugha ambayo ni rahisi kwa wahusika wote kuweza kuvielewa bila matatizo.

Aidha, kuna haja ya kuhakikisha kuwa wote waliopewa dhamana ya kusimamia viwango hivi hawaingiliwi katika kazi yao. Inabidi wizara zihakikishe kuwa kila darasa litakalojengwa kuanzia sasa litazingatia viwango hivyo na yeyote atakayekiuka amri hii achukuliwe hatua za kisheria.

Kwani bila kufanya hivyo itakuwa ni aibu na fedheha iliyoje kwetu iwapo miaka mitano ijayo tutaanza kushuhudia madarasa yaliyojengwa katika mipango ya kuendeleza elimu nchini yakianza kuporomoka moja baada ya jingine na pengine kusababisha maafa na pengine hata vifo vya walimu na hata watoto wetu!

Mitihani ishushwe daraja machoni mwa serikali na jamii

Na Robert Mihayo
Ilichapishwa 30 Januari 2007

Wiki iliyopita tulipata habari kuwa Serikali imewavua madaraka na kuwachukulia hatua za kinidhamu maofisa elimu 13 wa mikoa na wilaya na walimu 108 kwa kujihusisha na udanganyifu wa mitihani ya kumaliza elimu ya msingi mwaka jana.

Uamuzi huo ulichukuliwa baada ya tume iliyoundwa 2006 na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kubaini kuwa watumishi hao walijihusisha na udanganyifu.

Ni matumaini yetu kuwa adhabu hizi zimetolewa baada ya kufanyika uchunguzi wa kina uliothibitisha kuwa wahusika kweli walitenda makosa yale na kuwa walipewa fursa ya kujitetea kabla ya adhabu hizi kuchukuliwa dhidi yao.

Akitoa taarifa hizo, Waziri Margaret Sitta alisema kuwa uchunguzi huo umebainisha kuwa baadhi ya wazazi walihusika katika kutoa rushwa ili watoto wao wapewe majibu katika mtihani huo.

Tunampongeza Waziri Sitta na serikali kwa ujumla kwa hatua walizochukua dhidi ya tabia hii mbaya. Kwa kipindi kirefu uvujaji wa mitihani umekuwa tatizo sugu lakini bila hatua thabiti kama hizi za sasa kuchukuliwa. Kwa hiyo tabia hii inayotishia kuliangamiza taifa kielimu ilikuwa imeanza kuota mizizi na kujikita nchini.

Hatua kali iliyochukuliwa na Waziri Sitta ni mfano mzuri wa uwajibikaji na pengine ni mwanzo wa kuua ule utamaduni mbaya wa kuwalinda watenda maovu nchini kwa sababu tu ni 'Wenzetu'.

Lakini baada ya kuyasikia na kuyasoma yote haya inafaa tutulie na kujiuliza: hivi ni kwa nini wanafunzi, walimu, wazazi na wasimamizi wa mitihani wamejitumbukiza katika vitendo hivi viovu?

Kunaweza kuwa na sababu nyingi lakini kwa mtizamo wetu, moja ya mambo yanayochangia kuwapo kwa tatizo hili ni kuwa tumeufanya mtihani wa kumaliza darasa la saba kuwa kama ndiyo ufunguo pekee wa kuingilia peponi na kwamba mwanafunzi atakayeshindwa kufaulu mtihani huu atakwenda jehanamu. Mitihani ya kumaliza shule imekuwa ndiyo kigezo pekee kinachotumika kupima uwezo na maendeleo katika elimu ya msingi.

Hebu tumchukulie msichana anayemaliza darasa la saba mwenye matarajio ya kujiendeleza kimasomo. Kwake yeye kufaulu mtihani huu ni suala la kufa na kupona. Kwani asipofaulu kuna uwezekano mkubwa kuwa ataozwa na huo ndiyo kuwa mwisho wa ndoto zake za kujiendeleza kimasomo na kimaisha.

Hata kwa wazazi hali hii ya kuufanya mtihani wa mwisho kuwa ndiyo kigezo pekee cha kupima uwezo wa mwanafunzi kuendelea na masomo ya sekondari huleta msongo na hofu kubwa kwao na hivyo kulazimika kuchukua hatua zozote za halali lakini hata zisizokuwa za halali ili kuhakikisha kuwa mtoto wao anapenya kuingia sekondari!

Pengine tukiangalia kwa mtazamo huu tunaweza kufahamu ni nini kinachowasukuma watu hawa kufanya kitendo hiki kiovu.Tumekazania mno mtihani mmoja tu wa mwisho kuwa ndiyo ufunguo pekee wa kumwezesha mwanafunzi kuendelea na masomo ya sekondari.

Athari za tabia hii ziko nyingi.Kwanza, inasababisha kuwa na msongo na hofu kubwa kupita kiasi kwa wahusika wote kuanzia wanafunzi, wazazi na hata walimu.

Pili, huwalazimisha wanafunzi kuwa mabingwa wa kukariri; kwani aliye na uwezo wa kukariri ndiye atakayechaguliwa kuingia sekondari. Asiyekuwa bingwa wa kukariri hata awe na uwezo mwingine ambao kama vile kufikiri, kujenga hoja,udadisi ambavyo vinasaidia katika kutatua matatizo ya jamii hatachaguliwa aslani.

Ndiyo maana mwalimu anayewasaidia wanafunzi mara nyingi anaangalia mitihani ya nyuma na kuamua ni maswali yapi yatatolewa tena na kukazania kufundisha maeneo hayo, akijua hiyo ndiyo njia ya kuhakikisha anawapa nafasi nzuri wanafunzi ya kufaulu kwenda sekondari nay eye kusifiwa!

Tuonavyo sisi kuna haja ya kujifunza kutoka kwa wenzetu kuhusu njia mbadala za kupima uwezo wa watoto. Si sahihi kutumia mtihani mmoja tu wa mwisho kupima ubora wa mwanafunzi kuendelea na masomo ya juu. Kuna umhimu wa kumpima mwanafunzi kwa vigezo mbalmbali na kipindi chote awapo shuleni. Kwa mfano ufanisi wake katika mitihani ya mhula, uwezo wake kuchambua na kufikiri zaidi, kushiriki na ushirikiano na wenzake, uwezo wake wa kujenga hoja, kujiamini, kujieleza, kutatua matatizo n.k. Elimu ni uwezo wala si cheti pekee.

Kama Mwalimu Julius Nyerere alivyowahi kusema: "…shule zetu za msingi na sekondari ni lazima ziwatayarishe vijana wetu kukabiliana na hali halisi na mahitaji ya Tanzania; kufanya hivyo kunahitaji mabadiliko ya kimapinduzi, siyo tu katika mfumo wa elimu lakini pia katika tabia zilizojengeka katika jumuiya. Kikubwa inahitaji mitihani ishushwe daraja machoni mwa Serikali na jamii ..."

Pia Mwalimu aliwahi kutuasa: "Elimu inayotolewa ni lazima ijenge mambo matatu kwa kila mwananchi, akili ya kuuliza,uwezo wa kujifunza kutoka kwa wengine - na kuyakataa au kuyakubali kutokana na mahitaji yake - na uwezo wa kujiamini kama raia huru na sawa katika jamii…" Elimu ni uwezo, siyo cheti.

Baraza jipya lililoundwa kumshauri Waziri linabidi kumshauri kuhusu njia bora zaidi za kuwatahini wanafunzi. Mbinu zilizopitwa na wakati hazifai kupambana na changamoto za karne ya 21.

Ruzuku ya MMEM 2006/07: Maswali mengi yanadai majibu

Na Robert Mihayo
Ilichapishwa 13 Februari 2007

Hivi karibuni tumebaini kupitia magazetini kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) imetoa mgao wa fedha za ruzuku ya uendeshaji kwa halmashauri mbalimbali kwa kipindi cha mwaka 2006/07.

Hatua hii ni mhimu sana kwa sababu itaziwezesha halmashauri hizi kuzipatia fedha shule ili kukidhi gharama mbalimbali kama vile ukarabati wa madarasa, ununuzi wa vifaa vya shule kama vile vitabu vya kiada, madaftari, kalamu na chaki. Aidha, fedha hizi zinatarajiwa kuwawezesha walimu kuendesha shughuli za utawala wa shule zao kama vile kulipia gharama za mitihani n.k.

Umuhimu wa kuwa na vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia katika kuboresha elimu nadhani uko bayana. Ninawapongeza Wizara pia kwa kutoa matangazo haya kwenye magazeti ili kuyaweka mambo wazi.

Hata hivyo, baada ya kuipitia orodha ya mgao wa fedha nimejikuta maswali kadhaa yakiniijia kichwani mwangu.

Swali la kwanza ni kuhusu utaratibu uliotumika kutoa matangazo kupitia magazeti. Sina hakika kama kuna njia nyingine zitakazotumika kufikisha taarifa hizi mhimu kwa wadau wote wakiwamo walimu, wazazi, wanafunzi, maafisa elimu n.k. Kama haupo, nina hakika wadau wengi katika maeneo mengi ya nchi yetu watapata matatizo sana kuzipata taarifa kwa sababu hawapati kabisa magazeti.

Mathalani, hivi karibuni nilitembelea wilaya ya Kasulu Vijijini mkoani Kigoma.Wananchi wa kule hawapati kabisa fursa ya kusoma magazeti. Katika kijiji kimoja nilikuta gazeti moja tu la *Uwazi*. Ingawa gazeti lenyewe lilikuwa kuukuu la mwaka 2004, bado nakala hii ilikuwa imehifadhiwa vizuri ofisini kwa ofisa mtendaji wa kijiji kama rejea mhimu kwa wanakijiji kujisomea!

Sasa najiuliza walimu na wadau wengine wa maeneo kama yale watazipataje taarifa hizi mhimu? Hata watakapoletewa fedha hizi watawezaje kujua kama kweli hiyo ndiyo stahili yao kulingana na mpango wa MMEM?

Pili, kigezo kilichotumika kugawa fedha hizo kwa maeneo mbalimbali hapa nchini hakijawekwa wazi. Kuna tofauti kubwa sana kati ya wilaya moja na nyingine. Kwa mfano, kwa nini mwanafunzi wa wilaya ya Arumeru mkoani Arusha katengewa shilingi 4,500 wakati mwenzie aliyeko Ngorongoro mkoani humo humo anaambulia shilingi 1,500 tu?

Na kwa nini mwanafunzi katika wilaya nyingine kama Bariadi mkoani Shinyanga imetengewa ruzuku ya shilingi 100 tu? Hivi kiasi hiki kinatosha kununulia hata daftari? Na je, kwa nini wanafunzi wa shule zilizoko wilaya za Kasulu na Kibondo zote mkoani Kigoma na Nzega mkoani Tabora hawajapangiwa hata senti tano? Kwa nini kuna tofauti kubwa hivyo?

Aidha, kwa nini baadhi ya wilaya zenye wanafunzi wengi zimetengewa kiasi kidogo sana cha ruzuku zikilinganisha na zenye wanafunzi wachache? Mathalani ni vigumu kujua mantiki iliyotumika kuitengea wilaya ya Bukombe mkoani Shinyanga yenye wanafunzi 95,398 ruzuku ya shilingi milioni 286 wakati wilaya ya Bariadi yenye wanafunzi 146,343 inaambulia ruzuku ya shilingi milioni15 tu! Kuna haja ya kuviweka bayana vigezo vilivyotumika.

Tatu, haijawekwa bayana huu mgao ni kwa muda gani; mwezi mmoja, miwili, mitatu au sita? Na kama ni hivyo kuna kiwango kingine kitatolewa au kilishatolewa? Na ni lini? Kama ni kwa mwaka wote wa 2006/07, mbona ni kidogo mno ukilinganisha na sera? Kwa mjibu wa MMEM, kiasi kinacholingana na dola 10 za Kimarekani (takriban 13,000/-) kilipaswa kutolewa kwa kila mwanafunzi kila mwaka.

Iwe ni mgao wa mwezi mmoja, mitatu au hata wa mwaka; je wadau wamefahamishwa ni lini wategemee ruzuku nyingine na itakuwa kiasi gani? Bila hivyo Afisa Elimu na Mwalimu Mkuu wataweza kupanga mambo yao vizuri?

Nne, Wizara imeshawapangia halmashauri zote kiasi kipi kitatumika kwa mafungu mbalimbali: vitabu (40%); ukarabati (20%), daftari, kalamu, chaki (10%), n.k. Pengine Wizara imefanya hivyo kwa nia njema tu ya kuhakikisha kuwa masuala yote ya shule yanapewa pesa.

Lakini je ni busara kuwapangia watu vipaumbele vyao? Kwa mfano, unapozipangia wilaya zote kutumia 20% ya ruzuku yake kwa ukarabati huwezi kujua pengine kuna wilaya ambapo suala hilo si tatizo kubwa kiasi kile. Pengine kwao shida kubwa zaidi ni kupata vitabu na hivyo wangehitaji pesa zaidi kwa ununuzi wa vitabu badala ya kukarabati majengo!

Kwa nini walazimishwe kutumia pesa kwa kitu ambacho si cha muhimu kwao na kupewa kiasi kidogo kwa matatizo ambayo kwao yanahitaji kupewa kipaumbele zaidi? Nani anafahamu vizuri zaidi mahitaji ya shule; Katibu Mkuu Wizarani au walimu wa shule husika?

Aidha, utaratibu huu pia unaenda kinyume na ile dhana ya kuwezesha maamuzi yafanyike katika ngazi ya chini iliyoainishwa katika Mpango wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Na katika hili mlengwa zaidi ni mwalimu, mzazi na mwanafunzi. Si wangepewa fursa zaidi ya kuamua lipi hasa linalowakera shuleni kwao?

Kupeleka fedha shuleni ni jambo muhimu sana. Lakini bila utaratibu makini na wa wazi wa kugawa ruzuku, faida yake inaweza kuparaganyika.

Matokeo ya mtihani: Tunafurahia nini hasa?

Na Robert Mihayo
Ilichapishwa 20 Februari 2007

Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka jana yametangazwa. Kwa mjibu wa Katibu wa Baraza hilo, Dk. Joyce Ndalichako, kati ya watahiniwa 141,728 waliofanya mtihani huo,116,647 wamefaulu ikiwa ni asilimia 82.3 ya watahiniwa wote.

Matokeo hayo yanaonesha kuwa shule mbili za wasichana, St Francis ya Mbeya na Marian ya mkoani Pwani zimeongoza kwa kufanya vizuri mwaka huu. Lakini matokeo haya pia yanaonesha kuwa Zanzibar inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya shule zilizofanya vibaya.

Ni dhahiri kuwa kuna wale waliofurahishwa na matokeo haya kwa kuwa yamekuwa mazuri kwao. Lakini bila shaka kuna wale ambao yamewasononesha au kuwakatisha tamaa kwa kuwa yamekuwa mabaya, pengine kinyume na matarajio yao.

Katika kundi hili la pili pengine kuna mfano wa Pamela Alfred, mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya Adrian Mkoba Morogoro, aliyeamua kutoa uhai wake baada ya kuona kuwa matokeo yake yamekuwa mabaya kinyume na matarajio yake.

Kwa mjibu wa taarifa za vyombo vya habari, Pamela alikuwa miongoni wa wanafunzi nguli kitaaluma. Kwa hiyo, si yeye tu bali hata walimu wake pia walitarajia angepata daraja la kwanza kwenye mtihani huu. Lakini tofauti na matarajio, Pamela alipata daraja la mwisho kabisa; na hili ndilo lililomfanya Pamela kuchukua uamuzi wa kutoa roho yake!

Kwa jumla, matokeo ya mwaka huu yanatufundisha nini?

Kwanza, mfumo wetu wa kutathmini wanafunzi una kasoro nyingi. Tumeipa mitihani ya kumaliza shule umuhimu mkubwa kupita kiasi. Mitihani hii imekuwa ndiyo kigezo pekee kinachotumika kupima uwezo na maendeleo ya mwanafunzi.

Kwa kuufanya mtihani wa mwisho kuwa kama ndiyo ufunguo pekee wa kuingilia peponi kwa mwanafunzi na kwamba atakayeshindwa kufaulu atakwenda jehanamu kuna athari kadhaa. Huwafanya wanafunzi wengi kuingiwa na hofu kubwa. Ni kubwa kiasi cha kuwafanya hata baadhi ya wale ambao walitarajiwa hufanya vizuri kama alivyokuwa hayati Pamela, kuboronga katika mtihani wa mwisho.

Je, ni sahihi kutumia mtihani mmoja tu wa mwisho kupima ubora wa mwanafunzi? Je, tunaweza kumpima mwanafunzi kwa vigezo mbalimbali na kwa kipindi chote awapo shuleni?

Kama kungekuwa na utaratibu wa kuwapima wanafunzi kwa vigezo mbalimbali mathalani ufanisi wao katika mitihani ya mhula, uwezo wao kuchambua mada, uwezo wa kujenga hoja au kutatua matatizo n.k. kwa kipindi chote wawapo shuleni; huenda leo tusingekuwa tunaomboleza kifo cha Pamela!

Pili, matokeo ya mwaka huu pia yanatuonesha, kwa mara nyingine, kuwa shule za seminari ndizo zinaoongoza kwa kuwa na matokeo mazuri. Kwa mwaka huu, miongoni mwa shule kumi

zilizoongoza kwa kufanya vizuri, nane ni za seminari!

Tunapaswa kujiuliza, hivi ni kwa nini hasa shule hizi takribani miaka yote huongoza kwa kuwa na matokeo mazuri? Nini siri ya mafanikio yake?

Wakati huhuo inabidi pia tujiulize kwa nini shule za serikali, ambazo ndizo kimbilio la wanyonge wengi, huwa hazifanyi vizuri katika mitihani? Je, kuna mapungufu gani, na ni hatua zipi zinabidi kuchukuliwa kuidhibiti hali hii?

Lakini pia, ukiangalia vizuri matokeo haya utabaini kuwa miongoni mwa shule 10 zinazoogoza kwa kufanya vibaya, saba zimetoka Zanzibar! Swali ambalo linakuja mara moja kichwani ni, je, kuna matatizo gani katika mfumo wa elimu katika visiwa vya Unguja na Pemba?

Na, baada ya kuona tofauti hizi, hivi ni kweli kuwa watoto wote wa Tanzania wana fursa sawa ya kupata elimu bora? Kwa nini kijana wa Zanzibar au wa mzazi masikini asipate fursa sawa?

Tatu, matokeo haya yametuonesha, kwa mara nyingine tena, kuwa somo ambalo wanafunzi wengi (85.48%) wamefaulu vizuri ni Kiswahili. Hili ni jambo la kujivunia kwani inaonesha kuwa wanafunzi wengi wanaielewa vyema lugha ya Taifa letu.

Hata hivyo, matokeo haya pia yamebainisha udhaifu mkubwa walionao wanafunzi wengi katika somo la Hesabu kwani ni asilimia 23.1 tu ya watahiniwa wote ndio wamefaulu. Kwa maana nyingine, zaidi ya robo tatu ya watahiniwa walishindwa somo hili!

Matokeo haya yanasikitisha na kuleta hofu. Hesabu huwapa wanafunzi uwezo wa kufikiri kwa mantiki, na pia kudadisi na kujenga hoja. Kutokufanya vizuri kwa wanafunzi hawa ina maana wanakosa sifa hizi. Badala yake wanakuwa mabingwa wa kukariri tu!

Hesabu pia ni somo la msingi katika maendeleo ya sayansi na teknolojia katika taifa lolote. Sasa kama vijana wetu wanashindwa kulimudu, mustakabali wa taifa letu katika karne hii ya sayansi na teknologia utakuwaje?

Linalojitokeza hapa ni umuhimu wa kuuangalia upya mfumo wetu wa elimu na kuhakikisha kuwa tunawaandaa wanafunzi kukabiliana na hali halisi na mahitaji ya Tanzania. Kwa kuanzia, utaratibu wa kutathmini wanafunzi ubadilishwe kupima uwezo wa mwanafunzi na siyo ubingwa wa kukariri tu.

Je, viongozi wetu wana ujasiri wa kukabiliana na changamoto hilo?

Kulegeza masharti si dawa ya upungufu wa walimu

Na Nyanda Shuli
Ilichapishwa 3 Aprili 2007

Gazeti la Mwananchi la tarehe 26 Machi lilimnukuu kiongozi mmoja wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi akisema kuwa Serikali imelegeza masharti ili kuwapata walimu watakaoandaliwa kufundisha katika shule mpya zilizojengwa hivi karibuni. Hivyo, Serikali imeridhia vijana waliomaliza masomo ya sekondari (kidato cha sita) kuanzia 1998 na kufaulu (kwa kupata E na kuendelea) angalau somo moja la kufundishia kuomba kujiunga na mafunzo ya ualimu ya muda mfupi (wiki nne tu).

Siendekezi ubishi hapa. Kuna uhaba mkubwa wa walimu. Hii ni ishara kuwa hali si nzuri katika elimu ya sekondari. Kiongozi huyu alidokeza kuwa wizara ilitaka vijana 6,000 wajitokeze lakini ni 2,504 tu ndio waliokubaliwa mpaka sasa. Hawa wanatarajiwa kuokoa 'jahazi' katika shule za kata lakini pia alikiri kuwa shule za zamani zina upungufu mkubwa wa walimu.

Mwalimu ni nani? Katika taaluma ya elimu, mwalimu ni mwezeshaji wa wengine (wanafunzi) kujifunza. Mtazamo huu ndio unaosababisha mtu yeyote mwenye ufahamu wa mada fulani na amefundishwa (au ameelekezwa) namna ya kuwezesha wengine kujifunza anaweza kuwa mwalimu.

Wapo watu ambao wamemudu kuwa walimu wazuri lakini hawakupata mafunzo ya ualimu. Naamini kuwa wapo watu wenye vipaji binafsi vinavyowawezesha kufundisha. Kuna jambo moja liko wazi hapa. Pamoja na kuwa na vipaji binafsi, watu hawa lazima wawe na ufahamu wa kutosha wa masomo wanayofundisha.

Mtu ambaye hana ufahamu wa kutosha katika somo analotakiwa kufundisha, kamwe hawezi kuwa mwalimu mzuri. Kwa upande mwingine, wapo baadhi ya watu waliohitimu vizuri masomo ya ualimu lakini si walimu wazuri. Ni wachache ukilinganisha na wale ambao hawakuandaliwa vyema kufundisha, lakini wanafundisha.

Hivi sasa taaluma ya ualimu imevamiwa. Mtu yeyote anaweza kuwa mwalimu. Sijawahi kuona wataalam katika fani nyingine wanapatikana kwa njia za mkato. Kuna upungufu wa madaktari, manesi na wataalam katika fani nyingine pia. Inawezekana kuwapata kwa wiki nne? Kwa mfano kuhusu madaktari wa wiki nne, mtu atahoji: "si tutakufa?". Watoto wetu hawafi kifikra kutokana na walimu hawa wa chap chap? Hakuna kifo kibaya zaidi ya hiki. Hii ni sawa na kusomesha watu ambao hatutawatumia kuiendeleza Tanzania. Siombi itokee lakini naogopa kuwa baadae 'zao' la wanafunzi waliotokana na walimu wa hawa litadhihirika kutokana na ubabaishaji katika utendaji na uwajibikaji wao.

Siyo kila mtu anaweza kuwa mwalimu. Pamoja na mambo mengine, mwalimu anapaswa kuwa na sifa zifuatazo: Aweze kujiamini anapokuwa anafundisha. Hii itamwezesha kulitawala darasa, na wanafunzi watakuwa wasikivu kwake na kutilia maanani maelekezo yote anayowapatia.

Pili, mwalimu anapaswa kuwa na mbinu mbalimbali za ufundishaji. Afahamu kuwa wanafunzi darasani hawafanani. Wengine ni

wepesi kuelewa na wengine ni wazito. Ni jukumu lake kuhakikisha kuwa wote wanaelewa anachokifundisha. Mafunzo ya saikolojia yatamwongoza mwalimu kutambua uwezo wa wanafunzi na kuwasaidia.

Tatu, mwalimu anapaswa kupima uwezo wa wanafunzi na kuchochea maendeleo yao kitaaluma. Mwalimu aliyeiva anaweza kutambua vipaji vya wanafunzi. Kwa ujumla, elimu pia inapaswa kukuza vipaji vya wanafunzi katika fani mbalimbali kama michezo, uchoraji na sanaa nyingine. Sio kufuatilia tu masomo ambayo yametajwa katika mtaala na ambayo yatafanyiwa mitihani.

Nne, mwalimu ni mlezi pia. Anapaswa kuelewa kwa kina kuwa majukumu yake ni pamoja na kupandikiza maadili mema kwa vijana. Si kazi ya mwalimu fulani tu kukemea vitendo viovu vya wanafunzi, badala yake, walimu wote wanahusika.

Tano, pamoja na kazi ya kufundisha, mwalimu anapaswa kutoa ushauri kwa wanafunzi kuhusu masuala mbalimbali ya maisha, makuzi na masomo. Anapaswa kuwaongoza wanafunzi kuchagua masomo kulingana na vipaji vyao au taaluma ambazo wangependa kusoma hapo baadaye.

Hii inatosha kuonesha kuwa viongozi wa Serikali wanatakiwa kuwa makini katika kutafuta walimu. Kuendelea kupunguza masharti kwa lengo la kuwavutia watu wengi zaidi kuomba kujiunga na vyuo ni kurudisha nyuma taaluma nzima ya ualimu. Uamuzi huu unalenga kumpata mtu yeyote ambaye kakosa pa kwenda. Hii 'katu' haitokei kwenye fani nyingine. Kati ya mambo mengine, hii ni moja ya sababu zilizofifisha hata hadhi ya walimu katika jamii. Sababu kubwa ni kuwa watu wasio na sifa wanawekwa pamoja na walio na sifa ili kufanya kazi moja. Lakini wakati sisi tukiendelea kupunguza muda na masharti ya kuandaa walimu, Chama cha Walimu nchini Denmark kwa mfano kinaendelea na mazungumzo na Serikali yao ili kuongeza muda wa kufundisha walimu toka miaka minne na kuwa mitano!

Kuandaa walimu kwa wiki nne ni kuongeza ukubwa wa tatizo. Ni kuwaharibia wanafunzi mwelekeo wa elimu yao na maisha kwa ujumla. Wanahitaji walimu wenye uwezo. Pia kulegeza masharti na kuhitaji vijana waliofaulu japo somo moja ni hatari zaidi. Pengine Serikali ingefikiria namna ya kuwapa motisha walimu waliopo ili waipende kazi yao. Takwimu zinaonesha kuwa kuna walimu wengi wanaacha kazi kutokana na ugumu wa maisha na mazingira ya kufundisha. Hata walimu wapya wataendelea kukata tamaa kama hali ya maisha na mazingira ya kazi havitaboreshwa. Maandalizi makubwa yalihitajika kabla ya kujenga shule.

Je, walimu wetu ni wakombozi?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 22 Mei 2007

"Wale wenye wajibu wa kufanya kazi na vijana wa umri mdogo wana nguvu kubwa zisizozidiwa na nguvu za yeyote yule kwa kutilia maanani hali ya baadae ya jamii yetu. Nguvu hizi zipo katika makundi mawili-wazazi na walimu." Nyerere: 1966.

Haya ni maneno ya hayati mwalimu Nyerere aliyoyasisitiza sana wakati wa uhai wake. Je walimu tulio nao sasa ni wa aina gani? Wanalijengea taifa uwezo, mawazo na kulifanya mahali pazuri pa kuishi na penye maendeleo?

Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) linafafanua kuwa mwalimu ni muwezeshaji wa wanafunzi anayechochea fikira za wanafunzi. Mwalimu bora anatoa maarifa kwa kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri, kutenda, kubuni na kukabiliana na changamoto zinazowazunguka na hivyo kuleta maendeleo endelevu.

Hapa nchini, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inamtambua mwalimu kama mtu aliyefuzu mafunzo ya ualimu na kutunukiwa cheti au kibali maalum cha wizara ili akafundishe. Pengine walimu wetu wanahalalishwa na waraka huu. Lakini suala nyeti hapa ni je wana uwezo, sifa na umuhimu wa kuendeleza taifa kama anavyotuambia Mwalimu Nyerere? Kuwa na cheti cha kufundishia inatosha, hasa kama walimu siku hizi wanapigwa 'msasa' ya wiki mbili tu?

Kwa mtazamo wangu mwalimu mwenye uwezo huo anapaswa kuwa na sifa kuu tano muhimu za kiualimu:

Kwanza, ni mwenye maarifa na uwezo wa kutumia mbinu shirikishi kufundisha. Kufanya hivyo ni kuamsha na kuchochea fikira za wanafunzi ili waweze kufikiri zaidi na kuonesha uwezo walionao. Mwalimu ataweza kufanya hivyo pale ambapo anaheshimu mawazo ya watoto kwa kutambua kuwa nao wanajua na wanaweza kufikiri, siyo kuwaona kama makopo matupu ya kujazwa na busara za Mwalimu.

Pili, Mwalimu bora ni yule anayetambua mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia kutokana na uwezo wa wanafunzi, mazingira na aina ya somo, ili wanafunzi waelewe haraka na kujenga ufahamu, maarifa na uwezo wa kufikiri zaidi. Hili huambatana na ubunifu, uwezo wa kuthamini hatua za kujifunza na kuelewa, upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi na utambuzi. Pamoja na mwalimu mwenyewe kujitathimini kazi yake nzima ya kufundisha ili ajue udhaifu wake na hivyo kujiboresha zaidi kila wakati. Mwalimu asiye tambua mbinu na hatua za ufundishaji ni vigumu kutoa maelekezo sahihi kwa wanafunzi wake.

Tatu, ni mwenye fakra pevu na endelevu anayependa kujifunza, kujua zaidi na kuchambua masuala mbalimbali yanayoizunguka jamii na dunia. Na hivyo kuwa mpenzi wa kusoma kila wakati, na uwezo wa kusoma majira ya nyakati na kuyapokea mabadiliko chanya na kuyaepuka mabaya. Inampasa awe anapenda kusoma vitabu, majarida, magazeti, kusikiliza redio, kuhudhuria mikutano, na kuuliza maswali ya aina mabalimbali. Anafanya hivyo siyo kwa sababu kuna posho ya kuhudhuria semina

au atapandishwa cheo, lakini kwa sababu ni mpenzi wa kutaka kujifunza. Haya yatamfanya ajue masuala mapya yanayotokea katika jamii, na hivyo kupata utambuzi unaomjengea uwezo zaidi.

Nne, ni makini, na mwenye nidhamu ya kazi. Mwalimu bora hufika kwa wakati kazini, anaingia darasani na kufundisha kwa kutumia akili zake na mbinu zote, anayekamilisha majukumu yake kiusahihi na kwa wakati bila kusukumwasukumwa. Ni mtu mwenye upendo kwa watoto, asiye na makuu na mwenye wito na ari ya kufanya kazi kwa lengo la kuwajengea watoto uwezo wa kufikiri zaidi na kutenda.

Tano, tukumbuke fikra, mbinu za ufundishaji na maelekezo ya aina yoyote kwa mwanafunzi hayafikii wala hayawezi kulingana na athari za mwenendo au tabia ya mwalimu. Kwa maneno mengine matendo au mwenendo wa mtu ni rahisi sana kuigwa kuliko maelekezo yake. Mwalimu Nyerere alitukumbusha kwamba wanafunzi huwa wanasoma maisha na tabia ya mwalimu kuliko maelezo yake.

Mwalimu anayefundisha umuhimu wa kuheshimiana lakini mwenyewe ni mwepesi wa kutumia fimbo au lugha ya dharau kwa watu wa chini anafundisha dharau, siyo heshima. Mwalimu anayesisitiza nidhamu na uwajibikaji lakini katika maisha yake ya kila siku hajali na hawajibiki anafundisha uzembe, siyo uwajibikaji. Wanafunzi siyo wajinga, wanajua tofauti kati ya uwongo na ukweli halisi. Ila katika kujifunza wataiga na kufuata anachofanya mwalimu, na siyo kufuata anachosema mwalimu.

Pengine hii ndio siri ya ushindi wa shule nyingi za seminari na za binafsi ? Je hali hii inawezekana ni chanzo kikubwa cha kukosa uwezo na kushindwa kwa watoto wengi wanaotoka shule za serikali ?

Bila shaka kuna walimu wengi wazuri katika shule za serikali, wanaojitahidi kufanya kazi zao kwa wito na nidhamu. Lakini je, Wizara husika inafanya juhudi thabiti kuwatambua na kuwapa moyo ? Au hakuna tofauti kati ya yule anayefanya kazi na yule anayelipua ? Mwaka huu Rais Kikwete aliwatambua na kuwapongeza wanafunzi waliofaulu vizuri katika mitihani. Pengine mwakani angewatambua walimu bora – siyo tu wale wanaofaulisha wanafunzi, lakini wanaofundisha kwa kujali na kujituma kwelikweli. Walimu wanaowezesha wanafunzi wote kufikiri, kuuliza maswali, kuchambua, kubuni, kuthubutu na kujiamini. Kwa sababu hawa ndiyo walimu tanaowahitaji kujenga taifa letu.

Mzazi unachangiaje maendeleo ya mtoto?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 19 Juni 2007

Wazazi wengi wameitikia wito wa Serikali wa kuwataka wachangie ujenzi wa madarasa ili kuboresha elimu. Baadhi yao wanadhani huo ndio wajibu wao pekee ili kuboresha elimu ya watoto wao. Lakini je, lipi ni muhimu zaidi: kujenga jengo au kujenga mtu?

Katika kitabu chake, *Binadamu na Maendeleo*, Mwalimu Julius Nyerere aliliona hili na kusisitiza kuwa jamii inapaswa kutumia nguvu nyingi katika kumjenga mtu kwanza. Mwalimu alibainisha kuwa tukiwa na watu waliojengeka kielimu, ujenzi wa miundombinu yote utakuwa rahisi na wa ufanisi zaidi, na hatimaye taifa litaendelea haraka.

Mzazi anapochangia ujenzi wa shule, anatimiza wajibu wake kwa mtoto kwa asilimia 10 tu. Asilimia 90 iliyobaki ya wajibu wake ni kumjenga mtoto. Maana shule ya kwanza ya mtoto ni mafunzo na malezi bora toka kwa wazazi. Je wazazi wanaelewa hivyo?

Kwa mawazo yangu jamii na serikali ingetilia mkazo zaidi kuwajenga watoto kwanza ili kazi ya kuwaelimisha iwe rahisi zaidi na matunda ya elimu yalete maendeleo kwa Taifa. Wazazi wanaweza kumjenga mtoto kwa kufanya yafuatayo:

Kwanza, kumjengea mtoto uwezo wa kufikiri kwa kumsikiliza na kuthamini mawazo na utashi wake. Hii itamjenga mtoto kuwa mdadisi na mwenye kujiamini katika kutoa maoni yake kwa jamii. Wazazi wengi wanafanya kosa hili linalodumaza fikra, utashi, maarifa na kuzima uwezo wa mtoto. Si vyema kuwaziba midomo watoto kwa amri, sheria, na kanuni zisizokuwa na msingi.

Pili, ni kuchochea na kuamsha shauku za kujua na kujifunza kwa mtoto. Mara nyingi watoto wanakuwa na shauku za kujua na kujifunza mambo mengi. Mathalani, mtoto anaweza kuwa na shauku ya kuimba, kucheza, kuchora, kutunga, kubuni, kuongoza, n.k. Bila kuchochewa shauku hizi zinaweza kuyeyuka zote.

Mzazi anapaswa kumpatia mtoto muda wa kuonesha shauku zake na pia kumpatia vifaa vinavyoweza kumsaidia kufanya atakavyo, kama vile vifaa vya kuchorea, kuandikia na kuchezea. Anapaswa kuwa bega kwa bega na mtoto pindi aoneshapo shauku hizo; kwani shauku hizo ndizo kisima cha ujuzi na maarifa.

Tatu, kutambua uwezo na upeo wa akili ya mtoto; kutathimini maendeleo na ufanisi wake na kufuatilia kwa karibu maendeleo ya mtoto kimasomo. Mzazi anapaswa kujua ratiba ya mtoto wake ya shuleni na ya nyumbani. Pia anapaswa kuwajua walimu wake na mazingira anayojifunzia na hata kujua kiwango cha werevu na utambuzi wa mtoto.

Ingawa suala hili ni muhimu, wazazi wengi hawalipi kipaumbele na wamewaachia walimu tu. Kufuatilia na kutathimini maendeleo ya kielimu ya mtoto wako kunampa uhakika wa kutimiza malengo yake ya kujifunza.

Nne, kumsaidia mtoto kutekeleza dhana alizojifunza kwa vitendo. Kwa mfano, mzazi unaweza kumsaisdia mtoto aliyejifunza aina za mawe au udongo kwa

kumuonesha kitu halisi au kumpa hilo jiwe ashike. Hapa atatambua kuwa anachosoma ni uhalisia na kipo kweli, kuliko kubaki na dhana tu. Hii itamfanya mtoto apende kujifunza, atambue haraka na athamini kujifunza.

Tano, kuzungumza na mtoto mara kwa mara ili kujua namna anavyoyachukulia masomo na jinsi anavyojisikia anapofundishwa. Pia kujua mbinu inayomfanya aelewe zaidi darasani sambamba na kutambua ugumu au matatitzo yake katika kujifunza au kufundishwa. Hii inamwezesha mzazi kubuni njia mbadala za kumsaidia kufikia lengo.

Sita, kumjengea mtoto uwezo wa kuthubutu na kutenda kwa kumuhimiza kujaribu kila mara anapotaka kufanya hivyo. Pia kumpongeza mtoto anapofanya vizuri humtia moyo na kujitahidi kufanya vizuri zaidi. Hili huchochea ubunifu wa kutumia mbinu za aina mbalimbali kukabili changamoto zinazomzunguka manufaa yake na jamii.

Saba, kumsaidia mtoto kupanga malengo ya baadaye, kwa kuzingatia matakwa, mwelekeo na uwezo wake. Watoto wengi wanapenda aina fulani za kazi, biashara, ugunduzi, ufundi, uvumbuzi na hata ujuzi. Mzazi anaposhindwa kumsaidia na kumtia moyo, anampotezea mwelekeo wa maisha mwanae.

Nane, kumuelewesha mtoto juu ya umuhimu wa kushirikiana na wenzake na jamii kwa jumla. Ushirikiano huu unapaswa kuwa katika kazi za mikono na za kiakili, mijadala, uongozi na kutoa maamuzi. Hii inampa mtoto uwezo wa kutumia fursa, kupata ujasiri na stadi za kazi. Pia anapata mazoezi ya mwili, anajenga afya, akili na kupata ujuzi. Watoto wasiofanya hivyo hudumaa kifikra na hata afya zao huathirika.

Kwa kumalizia, inafaa wazazi waelewe kwamba watoto wao wana uwezo, matarajio na malengo ya kuwa watu muhimu katika jamii. Wanapokosa msaada wa wazazi uwezo matarajio na malengo yao hayo hutoweka. Je, mzazi unapenda kumuona mtoto wako aliyetaka kuwa daktari amekuwa mvuta bangi wa kijiweni?

Wazee vijijini hawajui umuhimu wa kusomesha wasichana?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 10 Julai 2007

Kampeni ya kuhakikisha watoto wanapata elimu imefichua ukweli kwamba wazazi wengi, hasa walio vijijini, wanasita au hata kukataa kabisa kuwapeleka shule watoto wa kike; hususani waliofikia umri wa kuolewa. Kutokana na hili Serikali pamoja na asasi nyingi zinalaumu wazazi hao kwa kushindwa kutambua na kuthamini elimu.

Wazee hao wanashutumiwa kwa kuthamini mahari, ngómbe au pesa kuliko elimu ya watoto wao. Tamaa ndiyo inadaiwa kuwasukuma kuwaoza watoto wao mapema.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) unabainisha kuwa, asilimia 28 ya mawaziri na asilimia 30 ya wabunge ni wanawake. Hii ilitokana na maamuzi ya wazee haohao kuwapeleka shule watoto wao wa kike. Matunda ya kusomesha wasichana ndiyo hayo jamii inayafurahia na kujivunia. Je, ni sababu zipi ambao zinawafanya wazee haohao sasa wathamini ndoa kuliko kuwapeleka wasichana shule?

Pengine kuna ushahidi mdogo wa kudharau maamuzi ya wazee kwani haujafanyika utafiti wa kutosha kutambua sababu za wazee kuwaoza watoto wao.

Inawezekana maamuzi ya kuwaoza watoto yanatokana na sababu nyingi zenye nguvu zaidi, kuliko hizi shutuma zinazoelekezwa kwa wazee. Kimsingi kila mzazi anapenda mtoto wake anufaike na awe mtu bora katika jamii. Anapoona alichokitarajia hakipo, hukata tamaa. Chanzo chake hasa kinaweza kuwa ni nini?

Moja, mzazi anampeleka mtoto shule akitarajia kuwa mwanae atajua kuandika, kusoma, kuhesabu na kusikiliza. Pia natarajia kuwa atapata uwezo wa kufikiri, kubuni, na kujitambua. Aidha, mzazi huyo anatarajia mtoto wake aliyeko masomoni atarudi na fikra mpya za maendeleo na ubunifu mkubwa wa kuyakabili maisha. Lakini watoto wengi, hususani wanaosoma katika shule za vijijini hawana stadi hizi. Hali hii huwavunja moyo wazazi.

Msichana anakaa shule miaka saba, lakini anahitimu elimu ya msingi akiwa hajui kusoma na kuandika vizuri, na hana stadi za maisha. Dada yake pia anahitimu kidato cha nne akiwa hawezi kueleza historia yake ya maisha kiufasaha. Hawezi hata kuelewa na kutafsiri aya fupi ya kiingereza chepesi. Na wala fikra pevu hazionekani kutoka kwake. Kwa hali hii tunapaswa kuwalaumu wazee wanaowaoza mabinti?

Pili, mzazi anampeleka binti shule, akitarajia mwanae atapata maarifa, ubunifu na uwezo. Na hivyo kutunukiwa vyeti vitakavyomsaidia kupata kazi. Au kujiajiri mwenyewe, na hatimaye kusaidia familia. Lakini kinyume na matarajio shule za vijijini watoto wengi hawapati kitu.

Matokeo yake badala ya kuwa msaada wanageuka kuwa mzigo tena katika familia. Huku michango, ada, sare, na matunzo yao shuleni vimewagharimu mno wazazi. Wazazi waliojidhiki ili watoto wao wasome. Nani asiyevunjwa moyo na hili?

Tatu, katika baadhi ya shule, wanafunzi wa kike wamegeuzwa kuwa vyombo vya starehe kwa walimu, vijana na viongozi wa vijiji wenye uchu wa ngono. Hili ni dhahiri kwa wengi maana ndiyo chanzo hasa cha ujauzito na mimba za wanafunzi tunazozisikia kila siku. Je, kipi ni bora; binti yako awe chombo cha starehe kwa walimu au upokee ng'ombe na aolewe?

Mzee anatarajia binti yake aliyeko shule arudi na maarifa ya kutosha na uwezo wa kuthubutu ili aisaidie familia na jamii kwa ujumla. Kinyume chake binti anarudi na ujauzito au UKIMWI kama zawadi kwa wazazi.

Pia, ni mzazi gani anapenda kuona mtoto wake anarudi na alama za viboko huku hakuna hata somo moja alilofundishwa siku nzima? Ni mzazi gani anayependa kuletewa shutuma za kushikwashikwa mtoto wake kila siku awapo shuleni au njiani kwenda shule? Na ni mtoto yupi ataipenda shule ya namna hii?

Nne, mazingira ya shule zetu za vijijini, hasa sekondari, bado ni magumu mno yasiyovutia wanafunzi kwenda kusoma, wala kuwashawishi wazazi kuwapeleka watoto shule. Mzazi gani anapenda kumwona binti yake anasoma shule isiyo na mabweni, maji, dawa au vifaa vya huduma ya kwanza? Ndiyo maana watu wenye uwezo, wakiwemo viongozi wa Serikali, hawawapeleki kabisa watoto wao kwenye shule hizo za kata.

Viongozi na watu wenye uwezo kifedha wanawapeleka watoto wao kwenye shule bora za kimataifa, binafsi au za dini. Kwa sababu zina mazingira mazuri sana ya kujifunzia, vifaa bora na vya kutosha na walimu bora. Na hivyo mtoto hupata anachotarajia.

Pengine ni muhimu zaidi kufikiria changamoto hizi kwanza kabla ya kukimbilia kushutumu wazee. Ni vyema kutambua kuwa aghalabu wazee wana busara; hivyo maamuzi yao siyo ya kubezwa bila ya kuyafanyia utafiti.

Iwapo mazingira ya shule, vifaa, walimu, ufundishaji na usalama vitaboreshwa, hasa katika shule za vijijini, wanafunzi watavutiwa. Wazee pia wataona umuhimu wa kuwapeleka shule mabinti wao; na katika halii hii yule atayekataa atakuwa amekosa hoja.

Elimu tele, lakini malengo yanafikiwa?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 7 Agosti 2007

Siku hizi viongozi wanatukumbusha kila wakati kwamba tuna elimu tele. Lakini malengo ya elimu yanafikiwa? Je, tuna elimu inayokidhi matarajio na matamanio ya mzazi, mwanafunzi na jamii? Elimu inayowawezesha vijana kupata stadi za maisha? Kuwa na uwezo wa kuyakabili mazingira, changamoto na kutatua matatizo yanayowazunguka?

Mihtasari ya elimu ya msingi na sekondari iliyotolewa 2005 na Wizara ya Elimu ya Tanzania, inabainisha malengo ya elimu Tanzania. Haya ni baadhi ya malengo na tathmini iliyofikiwa:

Moja, kupata stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na kuwasiliana kwa lugha ya kiswahili, Kiingereza na nyinginezo za kigeni. Je watoto wetu wanaohitimu wamepata stadi hizi?

Ni hali ya kawaida kuona baadhi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba hawajui kuandika wala kusoma. Hawezi kuhesabu wala kufanya hesabu ndogo. Hawezi kuwasiliana kiufasaha kwa lugha yeyote, na zaidi hawezi kabisa kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza. Hii sio kupingana na malengo ya elimu Tanzania?

Pili, kujenga ari ya kuendelea kujifunza. Wahitimu wetu inawezekana hawana ari ya kujifunza ndio maana wanakimbilia kuolewa, kuacha shule na hata kutafuta kazi ilihali wangali shule. Kukosekana kwa ari ya kujifunza kunatokana na nini?

Tatu, kujenga uwezo wa kufikiri kiyakinifu na kufanya maamuzi yenye mantiki. Je vijana wetu wanaweza kufikiri kiyakinifu na kuamua? Tunaona vijana wanahitimu na kurudi nyumbani hawana uwezo wa kutoa wazo jipya tofauti na aliloambiwa na mwalimu au alilosoma kwenye kitabu.

Hali hii inaweza kuwa inachangiwa na mbinu dhaifu za ufundishaji zisizochochea uwezo wa wanafunzi kufikiri. Bali zinachochea uwezo wa mwanafunzi kukalili na kupokea tu toka kwa mwalimu.

Nne, kutatua matatizo, kuwa mbunifu na kutumia mikono kuunda vitu anuai. Hili ni muhimu sana kwa dunia ya leo. Kila siku changamoto mpya zinaibuka katika jamii. Na vijana kama sehemu ya jamii wanapaswa kuwa na uwezo wa kutatua matatizo yanayowazunguka na kukabiliana na changamoto.

Mathalani, matatizo ya uharibifu wa mazingira, magonjwa, uhaba wa ajira na hata mahusianao katika jamii. Je watoto wetu wanaohitimu wanao uwezo huu?

Tano, Kutambua, kuheshimu na kupenda kufanya kazi. Je vijana wetu wa leo wanatambua na kupenda kufanya kazi? Wahitimu wengi wanaonekana hawana kazi na hawependi kufanya kazi. Imezoeleka kusikia na kuona vijana waliohitimu elimu ya msingi na sekondari hata vyuo wanakaa bila kazi.

Hawawezi kubuni hata mradi mdogo, kama vile ufugaji, kilimo, biashara, au ujasiriamali japo wengine wamesoma katika shule zenye miradi hiyo na taaluma hiyo. Wapo tu mitaani. Japo kuna misitu mikubwa, madini, wanyama, ardhi kubwa yenye rutuba, samaki baharini, madini, mazao ya misitu bado watu hawana kazi.

Kwanini lengo hili halifikiwi? Inawezekana elimu wanayopata ni dhaifu. Maana inawaandaa kupata cheti bila kupanda stadi za kupenda kufanya kazi na kuwa wabunifu.

Ukihoji wanafunzi kumi juu ya matarajio yao baada ya kuhitimu elimu yao, sidhani kama hata mmoja atasema anajiandaa kuanzisha biashara, mradi wa samaki, mbao, asali au kilimo cha kisasa. Sidhani hata mmoja anaweza kusema anafikiria kuvumbua, kugundua au kutengeneza kitu kipya.

Jibu rahisi kwa wengi nadhani litakuwa ni kupata cheti kizuri na kazi za ofisi. Je wabunifu na watu wanaofikiri katika nchi yetu watatoka wapi?

Tuendelee kutumia bidhaa zilizobuniwa na kutengenezwa na wageni toka kwenye malighafi zetu, huku tunaweza kuwaandaa wabunifu na watu wanaofikiri hapahapa?

Sita, kujielewa na kuheshimu utu wake, nafsi yake, utashi wake na nafasi yake katika jamii. Pamoja na uzuri wa lengo hili, tunaona ongezeko la vijana wanaotumia madawa ya kulevya,wanavuta bangi na kunywa pombe hadi kiwango cha kuvuruga akili zao.
Wanathamini madawa ya kulevya kuliko hata chakula?

Huu unaweza kuwa ushahidi kwamba elimu waliyopata haikuwafanya wajielewe, wajiheshimu na kuthamini utu wao. Kama wangepata elimu inayowafanya wajieshimu,watambue utu wao na nafasi yao kwenye jamii, wavuta bangi wangetoka wapi?

Inawezeka tukawa tunajidanganya kuwa malengo yanafikiwa kwa kuangalia uandikishaji na ujenzi wa majengo tu. Malengo ya elimu yanataka kujenga mtu na sio majengo kama mihutasari inavyosema.

Kuna faida gani kuwa na shule nyingi lakini wahitimu wako mitaani hawawezi hata kufikiri au kujitambua? Hadi wanaonekana wana chafua majiji na kustahili kuondolewa? Kuna faida gani kuwa na wingi wa wasomi wa vyeti tu wasioweza kufikiri wala kuthubutu huku tukiagiza wataalamu toka nje?

Hii ni hatari kwa jamii na taifa. Jamii inapokosa wabunifu haiwezi kuendelea, jamii inapokosa watu wanaofikiri, wanaothubutu, wanaotambua wajibu na nafasi zao kwenye jamii, haiwezi kuendelea. Pamoja na wingi wa mali na rasirimali nyingi tulizojaliwa bado maendeleo yatakuwa ndoto kama malengo ya elimu Tanzania yatabaki kwenye karatasi tu.

Mkataba wa KADCO ni kejeli kwa demokrasia?

Na Kajubi Mukajanga
Ilichapishwa 8 Agosti 2006

Dola ya kisasa ina nguzo tatu: Utawala, Bunge na Mahakama. Kisa cha kuwa na nguzo hizi ni kuhakikisha kunakuwepo udhibiti na ulinganifu katika matumizi ya madaraka katika mchakato wa kuendesha nchi.

Mpangilio huu ndiyo msingi wa demokrasia. Ikiwa nguzo moja itahujumu uhuru wa nyingine kutekeleza majukumu yake, basi demokrasia inakuwa imehujumiwa. Na ikiwa nguzo mojawapo itashindwa kumaizi na kutumia madaraka yake kwa manufaa ya umma, basi demokrasia inakejeliwa.

Hivi karibuni kumekuwa na mjadala Bungeni kuhusu mkataba wa uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Mjadala huu umeibua mashaka makubwa kama maslahi ya nchi yalizingatiwa katika mkataba kati ya kampuni ya Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO) na Serikali.

Wabunge walihoji faida ambayo taifa linapata kutokana na mkataba huu uliofanya uwanja huo ukabidhiwe kwa kampuni binafsi. Naibu Waziri wa Miundombinu, Mama Maua Daftari, akaeleza kuwa pamoja na mambo mengine, KADCO imetumia zaidi ya shilingi bilioni saba katika ukarabati na ujenzi wa miundombinu na vifaa hapo uwanjani, pamoja na mafunzo kwa wafanyakazi.

Majibu waliyopata wabunge hayakuwaridhisha. Kuna wananchi ambao wamekuwa wakitaka kujua ikiwa kweli Serikali inalipwa dola elfu moja tu kwa mwezi. Wabunge wakaambiwa Serikali imebaki ikimiliki hisa asilimia 24, na kwamba mkataba huo ni wa miaka 25.

Bado wabunge hawakuridhika, hivyo wakaomba mkataba uletwe Bungeni waudurusu. Na hapo ndipo walipopata mshangao wa mwaka. Wakaambiwa kuwa Kifungu 30(4) cha mkataba huo kinazuia mtu yeyote ambaye hahusiki moja kwa moja katika utekelezaji wake kuuona. Kwamba ndani ya mkataba, kuna kifungu kinacholizuia Bunge kuuona mkataba!

Mheshimiwa waziri akawaeleza wabunge kwamba "Serikali inaweza kupata taarifa kwa niaba ya Bunge".

Lakini tunawezaje kusema Bunge halihusiki na mambo ya mkataba huo, au mwingine wowote? Wabunge ndiyo wawakilishi wa wananchi. Ikiwa wao hawahusiki na masuala ya mikataba inayohusu rasilimali za taifa, basi anayemiliki mali hiyo ni nani?

Katiba ya Tanzania inaeleza kuwa Bunge litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge. Kisha Kifungu 63(2) kinasema sehemu ya pili ya Bunge, yaani Wabunge, "itakuwa ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, **kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano** na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."

Aidha, Kifungu 63(3)(c) kinaelekeza kuwa kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza "kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa

kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo."

Ikiwa hivi ndivyo, vipi tunakuwa na mikataba yenye vifungu vinavyolizuia Bunge kuihoji? Huku sio kwenda kinyume na Katiba? Na je, mkataba unaokwenda kinyume na matamshi na dhamira ya Katiba ni halali?

Je, kusema sehemu moja ya dola ambayo ni Utawala itapata habari za KADCO "kwa niaba ya Bunge" siyo kusahau kanuni ya kutenganisha madaraka? Siyo kusahau kwamba sababu ya kuwa na nguzo tatu ni pamoja na ili kila moja "imchunge" mwenzie?

Kulizuia Bunge kuhoji utendaji wa serikali, ikiwa ni pamoja na mkataba wa KADCO au mikataba mingine kuhusu mali ya umma, ni kuikejeli demokrasia. Mashirika ya kiraia na yasiyo ya serikali, vyombo vya habari, na wabunge wenyewe, tunafanya nini kuhusu jambo hili? Na wewe msomaji je?

Uongozi ni utumishi, si ubwana

Na Kajubi Mukajanga
Ilichapishwa 12 Septemba 2006

Hivi karibuni kumekuwa na habari njema kutoka kwa viongozi wakuu mintarafu upelekaji madaraka kwa umma. Rais Jakaya Kikwete ameongelea umuhimu wa wakuu wa wilaya kutohodhi madaraka ya halmashauri, na Waziri Mkuu Edward Lowassa akatolea ufafanuzi majukumu ya madiwani kama wadhibiti wa halmashauri.

Rais Kikwete, akijibu hoja za wajumbe katika semina elekezi ya wakuu wa mikoa, wilaya na makatibu watendaji huko Ngurdoto, aliripotiwa akiwaambia viongozi hao kwamba hawezi kuwanyang'anya wananchi mamlaka yao na kuwapa wakuu wa wilaya, kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na misingi ya demokrasia na utawala bora.

Kwa mujibu wa Mwandishi Msaidizi wa Rais, Maura Mwingira, Rais alisema wakuu wa wilaya hawawezi kuwa na nguvu kuliko halmashauri za wilaya zenye mamlaka inayotokana na wawakilishi wa wananchi.

Alisisitiza kwamba mkuu wa wilaya hawezi kuwa na mamlaka ya kila kitu kwani hiyo itakuwa sawa na kumpa mamlaka ya veto, na akasisitiza kwamba ni makosa kwa viongozi hao kujiona kuwa wao ni bora zaidi kuliko watu wengine.

Matamshi haya ya Rais ni ya muhimu sana. Sio tu kwa kuwa yeye ni kiongozi mkuu wa nchi, bali vile vile kwa kuwa watu aliowaambia hayo ni wawakilishi wake mwenyewe huko wilayani.

Rais, kwa kutamka hayo, amekumbusha umuhimu wa kanuni ya kutenganisha madaraka kati ya mihimili ya dola, ambayo ni utawala, uwakilishi na mahakama.

Msisitizo wa Rais umekuja wakati muafaka kwani nchi iko katika jitihada za kupeleka madaraka kwa wananchi. Lengo hili haliwezi kufanikiwa ikiwa viongozi hawataielewa na kuikubali kwa vitendo dhana hiyo.

Msisitizo wa Rais ni muhimu pia kwa kuwa unavunjilia mbali dhana ya kwamba busara ni hodhi ya watawala pekee. Kwa kukataa kuwafanya wawakilishi wake kuwa miungu-watu, Kikwete pia amekumbusha kwamba uongozi bora ni ule unaozingatia kwamba uongozi ni utumishi, si ubwana.

Kumekuwa na malalamiko kwamba wakati mwingine halmashauri haziendeshwi vyema na wakuu wa wilaya wanashindwa kuchukua hatua za kufaa kwa kuwa hawajapewa meno ya kufanya hivyo.

Malalamiko kuhusu udhaifu katika utendaji yanaweza kuwa na ukweli, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kuvunja misingi ya demokrasia na utawala bora.

Na hapa ndipo kauli ya Waziri Mkuu inapokuwa na umuhimu wa pekee katika suala hili. Akifungua semina elekezi kwa viongozi wa mkoa wa Dodoma hivi karibuni, Lowassa aliwataka madiwani nchini kuhakikisha kwamba uendeshaji wa mamlaka za serikali za mitaa unaondokana na kasoro ambazo zimekuwa zikijirudia mwaka hadi mwaka.

Aliwataka madiwani kuwa makini na kusimamia matumizi ya halmashauri ili

kuhakikisha rasilimali za halmashauri zinatumika kwa kazi zilizopangwa.

Alisisitiza kwamba madiwani lazima wabadilike na kuondoa ugoigoi wa utendaji katika halmashauri kwa kukagua miradi ya vijiji na kujiridhisha juu ya utekelezaji wake na matumizi ya fedha za walipa kodi.

Kauli ya Waziri Mkuu imesaidia kujibu maswali ya wale wanaolalamika kwamba kuna udhaifu katika utendaji wa halmashauri na kwamba wakuu wa wilaya wawezeshwe kuushughulikia.

Lowassa ameweka bayana, ikiwa ilikuwa haieleweki vyema, nani msimamizi wa halmashauri. Ni madiwani. Alisema madiwani ni wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kidemokrasia kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kimaendeleo na kwa maana hiyo, wao ndiyo wanaounda halmashauri za serikali za mitaa.

Kauli ya Rais na ile ya Waziri Mkuu zinatoshelezana. Kwa upande mmoja, Rais amewakumbusha wawakilishi wake umuhimu wa kuodokana na mawazo ya kwamba wao ndiyo wao tu, akawakumbusha kwamba wao ni watumishi; na kwa upande mwingine, Waziri Mkuu amewakumbusha madiwani kwamba wana jukumu muhimu la kuhakikisha halmashauri zinafanya kazi na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Wakati mmoja ameonya dhidi ya mwelekeo wa kutamani kuhodhi madaraka, mwingine amekumbusha umuhimu wa kutimiza majukumu kwani kufanya hivyo ndiko kunawapa uhalali madiwani na halmashauri.

Mwendo ukiendelea hivi, na viongozi wa ngazi za chini nao wakiwa na mtazamo huu, misingi ya utawala bora itajengeka na bila shaka maendeleo na demokrasia vitajengwa kwa kasi zaidi.

Wakuu wa wilaya na madiwani ni washirika katika harakati za maendeleo. Wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja, kwa kuheshimiana, na kila upande ukielewa majukumu na mipaka ya mwenzie. Kila upande unapaswa kutimiza wajibu wake, na kila upande unapaswa kumsaidia mwenzake. Wote ni watumishi wa wananchi.

Dhana imeeleweka, utekelezaji je?

Kuwapa taarifa wananchi si hiari, ni lazima

Na Kajubi Mukajanga
Ilichapishwa 3 Oktoba 2006

Serikali inaingia mkataba na kampuni ya kigeni wa miaka 40 wa kutafiti na kuchimba mafuta. Nani ana haki ya kujua yaliyomo katika mkataba huo? Mengi ya mashirika ya umma takriban 400 aliyoacha Mwalimu Nyerere ama yameuzwa au kufilisika. Mwananchi ana haki ya kuuliza na kupewa taarifa?

Akifungua warsha ya viongozi juu ya mawasiliano na umma kuhusu sera za Serikali hapo Machi 18, 2003 mjini Bagamoyo, Rais Benjamin Mkapa alisisitiza umuhimu wa wananchi kujulishwa sera na mipango ya serikali.

Rais Mkapa alisema kuwasiliana na umma kuhusu sera za serikali ni jambo muhimu katika ujenzi wa utawala bora. Na utawala bora, aliongeza, unazingatia ushiriki wa wananchi, lakini ushiriki makini ni ushiriki wa watu wenye taarifa.

"Jukumu la kuwasiliana na wananchi sio hiari; ni wajibu, na ni lazima", Rais alisisitiza.

Naye Rais Jakaya Kikwete, akizindua Bunge jipya Desemba 30, 2005, aliwaambia wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba wategemee serikali itakayoendeshwa kwa misingi ya utawala bora, itakayozongatia uwazi na uwajibikaji.

Aliapa kwamba serikali yake itapambana kikamilifu na ufisadi, na kwamba manunuzi na mikataba mikubwa itawekwa wazi.

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) pia unasisitiza umuhimu wa serikali iliyo wazi. Nguzo ya tatu ya MKUKUTA ni Utawala Bora na Uwajibikaji. Moja ya matarajio chini ya nguzo hii ni kwamba viongozi na watumishi wa umma watawajibika kwa wananchi kutokana na kupungua kwa ufisadi na upatikanaji habari kwa umma.

Juu ya hapo, Ibara ya 18 ya Katiba ya Tanzania inaweka wazi haki ya raia kuwa na uhuru wa kutoa na kupokea maoni na habari muhimu kuhusu maisha yake.

Yote haya maana yake nini? Maana yake ni kwamba muda umefika wa kuchukua hatua madhubuti za kutafsiri sera, matamshi ya viongozi wetu wakuu, na matakwa ya katiba katika vitendo.

Pamoja na kuzingatia ukweli kwamba kila serikali ina siri inazopaswa kutunzwa walau kwa kipindi fulani kwa ajili ya usalama wa nchi, tunahitaji kuchukua hatua za makusudi kabisa za kurahisisha upatikanaji wa nyaraka za serikali kama njia ya kupanua uwazi serikalini.

Pamoja na mambo mengine, upatikanaji wa taarifa za serikali utasaidia kuhamasisha ushiriki wa wananchi; kujenga mawasiliano kati ya wananchi na serikali; kuwawezesha wananchi kufanya maamuzi ya busara katika masuala muhimu; na kuipa serikali mrejesho kutoka kwa wananchi, mashirika ya kiraia, vyombo vya habari na wasomi.

Uwazi utasaidia pia kuondoa udhaifu wa kiutendaji katika utumishi wa umma kwani watumishi wataondokana na tabia ya kuwapuuza wananchi. Watumishi watajali zaidi majukumu yao. Aidha, uwajibikaji utajengeka.

Serikali ya awamu ya nne tayari imeanza kuonyesha nia hii kwa vitendo. Katika semina elekezi kwa viongozi zilizofanyika Ngurdoto, Rais Kikwete amesisitiza sana viongozi kuwa watumishi na si mabwana. Ametaka viongozi wawasiliane na wananchi, na kuwasikiliza.

Serikali imeanzisha tovuti kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi. Hotuba za Rais na mawaziri zinachapishwa katika ukamili wake magazetini. Waziri wa Habari ameahidi Bungeni kuwa serikali itakamilisha muswada wa uhuru wa habari hivi karibuni. Ameahidi vile vile kufungua ofisi mpya tano za Idara ya Habari katika mikoa ya mpakani ya Kigoma, Mtwara, Mbeya, Mwanza na Rukwa. Tunapongeza sana jitihada hizo.

Hata hivyo, tunadhani jitihada zaidi zinahitajika ili kufikia lengo mapema. Tunapendekeza yafuatayo:

Kwanza, nyaraka zote za serikali zichapishwe katika Kiswahili, badala ya mtindo wa sasa ambapo nyingi ziko katika Kiingereza. Zilizo katika Kiingereza zitafsiriwe.

Pili, nyaraka zote ziwekwe katika tovuti ya serikali ndani ya wiki moja tangu kutolewa kwa nyaraka hizo. Hali kadhalika, nyaraka zipelekwe katika maktaba za umma na vituo vya habari mbalimbali nchini, vikiwamo vile vya walimu.

Tatu, katika ngazi ya mtaa na kijiji, mbao za matangazo zitumiwe kikamilifu kutangaza nyaraka, mipango na shughuli za serikali.

Nne, nyaraka muhimu zitumwe kwa kila mbunge mara zinapotoka. Jambo hili lifanyike bila ucheleweshaji na liwe ni suala la utaratibu na siyo mapenzi binafsi ya watendaji.

Tano, mikataba ya Huduma kwa Wateja iliyoandaliwa na wizara, idara na mamlaka mbali mbali itangazwe ili wananchi waelewe kuwa wana haki ya kupata huduma gani ndani ya muda gani, ili waweze kudai zao.

Sita, mashirika ya hiari na yasiyo ya kiserikali yasambaze nyaraka za serikali ikiwa ni pamoja na kutafsiri sera katika lugha rahisi itakayoeleweka kwa wengi.

Saba, mchakato wa kuandaa muswada wa sheria ya uhuru wa habari (Freedom of Information Act) uongezwe kasi na uwe shirikishi. Sheria hii itaondoa hali ambapo utoaji habari unategemea matakwa ya afisa binafsi serikalini.

Nane, kila wizara, idara na mamlaka iajiri afisa habari na mahusiano ya umma ambaye atahakikisha kuna mawasiliano kati ya wizara, idara na mamlaka kwa upande mmoja na wananchi kwa upande mwingine. Vyombo vya habari pia vitumike kikamilifu.

Haya yote yanawezekana ikiwa kuna nia. Na mti utaujua kwa matunda yake. Uthibitisho wa udhati wa viongozi wetu utaonekana katika utekelezaji wa yale wanayoahidi.

Mageuzi polisi jamii yaungwe mkono kwa vitendo!

Na Lilian R. Kallaghe
Ilichapishwa 19 Desemba 2006

Ninapofungua magazeti na redio mara kadhaa nakutana na habari zifuatazo: Polisi wapambana na majambazi. Wezi wafunga mtaa na kupora mali za wananchi. Vibaka wavamia maduka. Mtoto amebakwa. Mtuhumiwa auawa na 'wananchi wenye hasira'. Akamatwa kwa rushwa nk. Haya ni baadhi ya matukio ya uhalifu ambayo polisi anatakiwa kukabiliana nayo kila siku.

Nalinganisha matukio hayo na safari yangu siku moja nilipotembelea makazi ya Polisi. Hii ilitokana na mwaliko wa mmoja wa ndugu yangu ambaye ana uhusiano wa karibu na askari polisi mikoani. Wenyeji waliandaa vinjwaji nje, chini ya mti kwani ndani ya nyumba hizo za bati au (*full suit*) kama walivyoziita, hapakukalika kutokana na joto kali lililokuwa ndani! Ilinikumbusha miaka ya themanini, nilipokuwa jeshi la kujenga taifa.

Hali katika makazi hayo kwa kweli ilinisikitisha! Nyumba zilikuwa ndogo. Zimebanana na baadhi ya familia jirani zilikuwa zikitumia jiko na hata choo kimoja! Mazingira yalikuwa masafi, lakini msongamano wa watu na watoto ulipafanya mahali hapo kukosa mvuto.

Nilijiuliza maswali mengi. Hivi haya kweli ndiyo makazi ya polisi tunaotarajia watulinde na mali zetu? Hawa ndio tunaotarajia wahatarishe maisha yao kwa ajili yetu? Kwanini mahitaji yao yasipewe kipaumbele kama baadhi ya watendaji kwenye taasisi za serikali? Kwanini wanaachwa waishi katika mazingira haya mabovu? Iweje tunatumia mabilioni ya shilingi kujenga na kukarabati majengo ya kifahari ya taasisi za serikali badala ya nyumba za walinzi wa maisha na mali za walipa kodi?

Nimekuwa pia nikifuatilia matatizo mengine yanavyoainishwa katika vyombo vya habari. Mishahara midogo. Vitendea kazi duni ambavyo haviendani na hali ya uhalifu wa karne hii. Kukosa usafiri na hata simu kwa ajili ya mawasiliano katika vituo mbalimbali nchini. Ni kawaida kumwona askari wa usalama barabarani akiongoza magari wakati wa mvua kubwa bila kuwa na koti la kujikinga!

Polisi ni nani na nini wajibu wao? Kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Ofisa wa Polisi, Polisi ni wananchi wenzetu wenye wito kulinda maisha na mali ya wananchi wenzao. Jukumu lingine ni kuwalinda wasio na hatia dhidi ya ugandamizaji, vitisho, vurugu, udanganyifu na kuheshimu haki za kikatiba za 'raia' wote.

Niliwahi kuaswa na mmoja wa makamanda wa polisi kwamba; "kusema *raia na polisi* ni sawa na kuwatenga polisi na kuonesha kuwa wao si raia wenzetu! Ni kama kusema polisi ni raia wa nchi nyingine... imezoeleka hivyo lakini si sahihi!"

Kutokana na majukumu makubwa tuliyowapa polisi wetu, je tunawasaidia vipi? Ni kweli kwamba uongozi wa serikali ya awamu ya tatu ulitoa ahadi za kuboresha hali katika jeshi hilo. Nyumba za kuishi katika baadhi ya vituo vya polisi zilijengwa ingawa ni chache mno, na sina shaka ni kwa ajili ya baadhi ya viongozi wa vyeo vya juu.

Vilevile kumekuwa na mabadiliko makubwa tangu kuchaguliwa kwa mkuu

mpya Inspekta Jenerali Saidi Mwema. Tumeona jinsi ambavyo jeshi hilo limejipanga upya kupambana na uhalifu wa aina mbalimbali na hivyo kurejesha hali ya usalama, hasa jijini Dar es Salaam.

Katika zunguka yangu nimeshuhudia pia mabadiliko yafuatayo: Vitendea kazi kwenye baadhi ya vituo vya polisi vimeongezeka, japo kidogo. Kutangazwa kwa namba za simu za viongozi wa juu wa polisi kumerahisisha ufuatiliaji wa matatizo ya wananchi. Pia utendaji kazi wa baadhi ya askari umebadilika. Si wote lakini wengi wanajali na kusikiliza matatizo ya wananchi bila ubabaishaji.

Mabadiliko mengine yanayofanywa na jeshi hilo ni kuligeuza kuwa Polisi Jamii. Kwa mujibu wa taarifa kupitia vyombo vya habari, lengo ni kufanikisha utendaji kazi wa polisi kwa kushirikiana kwa karibu na wananchi. Hiyo ni hatua muhimu kwa sababu bila ushirikiano na wananchi, polisi peke yao hawawezi kutekeleza wajibu wao.

Licha ya kuungwa mkono na wananchi, juhudi za Jeshi la Polisi haziwezi kufanikiwa bila kuwa na utashi wa kisiasa kutoka kwa viongozi kama vile wabunge na mawaziri. Je, mawaziri na wabunge wataunga mkono juhudi za Inspekta Mwema kwa vitendo na kwa kuzingatia muundo wa Polisi Jamii?

Mabadiliko yanayofanywa na jeshi hilo yasigeuzwe kuwa ya kisiasa kwani polisi ni watendaji wataalam wanaoielewa kazi yao kwa mujibu wa kanuni na sheria za nchi. Bila shaka polisi wanawajibu kufanya kazi yao kwa kuzingatia maadili na haki za wananchi. Lakini kufanikiwa, wanahitaji kuungwa mkono na wanasiasa *(political support),* kutengewa fedha za kuboresha mazingira ya kazi na makazi yao, kusikilizwa wanapotoa hoja zao kwa viongozi na kusaidiwa kwa vitendo. Bila hayo, nachelea kusema kuwa haki za binadamu, amani na utulivu tunavyojivunia tutakuwa tunaviweka rehani.

Rais anahitaji washauri wa aina gani?

Na Rakesh Rajani na Robert Mihayo

Ilichapishwa 6 Machi 2007

Makala ya gazeti moja hivi karibuni ilielezea wasiwasi wake kuhusu kauli za utatanishi ambazo zimekuwa zikitolewa na Rais Jakaya Kikwete na hatimaye zinakuja kudhihirika kuwa si za kweli.

Mfano wa karibuni ni kuhusu sakata la rada inayoihusisha kampuni ya BAE System ya Uingereza iliyoiuzia Tanzania rada hiyo. Mara kadhaa na katika sehemu mbalimbali, Rais Kikwete amekuwa akinukuliwa akisema kuwa kampuni hiyo inamilikiwa na Serikali ya Uingereza. Lakini tofauti na kauli hizi za Rais Kikwete, hivi majuzi Ubalozi wa Uingereza nchini ulitoa taarifa ukisema kuwa Serikali ya Uingereza haimiliki kampuni hiyo!

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Rais wetu kutoa kauli zenye utata namna hii. Alipokuwa akizungumzia sakata la filamu ya *Darwin's Nightmare*, Rais aliripotiwa kutamka waziwazi kuwa 'hakuna mtu anayekula mapanki'. Kauli hii iliwashangaza wananchi, hususan wale waishio Kanda ya Ziwa, kwa sababu wengi wao wamekuwa wakila mapanki kama kitoweo kwa miaka mingi sasa.

Pia, Rais aliwahi kutoa kauli mara mbili tofauti kuhusu matangazo ya luninga aliyodai kuwa yalitolewa na shirika la HakiElimu kuhusu UKIMWI na rushwa mahakami, wakati moja ilikuwa ya Femina na nyingine ya TAMWA.

Mwandishi wa makala aliona hali hii inasikitisha na kututia aibu, na aliuliza: Inawezekanaje Rais wetu awe akitoa kauli zenye mkanganyiko wa namna hii hata kwa vitu ambavyo havina utata na vinafahamika baada ya utafiti wa kawaida? Je, ni nani anayemshauri Rais wetu?

Yale anayotamka Rais yanatakiwa kuwa ya kweli kwani anayoyasema ni kwa niaba ya watanzania. Yeye ndiye sauti yetu na pia ndiye mhabarishaji wetu mkuu. Kwa hiyo kila anachokitamka lazima kwanza kiwe kimefanyiwa utafiti kabla ya kutolewa hadharani.

Mawaziri na washauri wa Rais ni watu muhimu sana; kwani wao ni kiungo kati ya Rais na jamii. Kwa hiyo kwa upande mmoja, wanapaswa kumfahamisha Rais ukweli mtupu kuhusu masuala yanayoikabili nchi na wananchi wake, hata kama ukeli huu ni wa kuudhi au kukera namna gani.

Kwa kufanya hivi watamwezesha Rais wetu kupata picha sahihi ya yale yanayoikabili nchi. Kwa kupewa ukweli huu Rais muda wote atakuwa amewezeshwa kufahamu hali halisi ya matatizo ya nchi na ya wananchi wake. Kwa hiyo Rais anakuwa na fursa nzuri zaidi ya kutoa uamuzi muafaka kwa matatizo hayo.

Kwa upande mwingine, baada ya kumpa hali halisi ya masuala husika, wasaidizi wa Rais tunadhani pia wana wajibu wa kumshauri Rais kuhusu njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kutatua tatizo hilo. Rais si malaika ambaye anajua kila tatizo na jawabu lake. Ni wajibu wa wasaidizi wake kumfahamisha yale yaliyo muhimu na pia kumpa njia mbadala za kuyatatua, ingawa yeye ndiye mwenye uamuzi wa mwisho.

Hatuna hakika sana kama mawaziri na washauri wengine wa Rais wanatambua dhima hii kubwa waliyonayo kama viungo mhimu kati ya Rais na watanzania anaowaongoza. Tunasema hivi kwa sababu ya mifano iliyotajwa juu, na pia kutokana na Rais mwenyewe kusema wazi kuwa amechoka na sifa za uongo. Mara kwa mara Rais amezingatia anapenda viongozi, bila shaka na yeye mwenyewe akiwemo, kukosolewa. Tarehe 13 Machi, 2006, katika semina elekezi ya viongozi huko Ngurdoto, Rais Kikwete alisema:

> "Siri ya kufanikiwa kufanya hayo ni kwa sisi viongozi kuwa tayari kufanya uchambuzi wa ukweli kuhusu hali ilivyo na kuwa tayari kukiri mapungufu. Vilevile, tuwe wepesi kufanya masahihisho. Nawasihi tuitumie fursa hii kufanya hivyo kuhusu uongozi na utendaji Serikalini. Kiongozi mzuri ni yule ambaye yuko tayari kujikosoa na kukosolewa. Mwongozo wa TANU unatukumbusha kuwa kujikosoa si kitendo cha kujidhoofisha bali ni kitendo cha kujiamini na kujiimarisha."

Je, wasaidizi wa Rais wanaogopa kumshauri kwa kusema ukweli? Pengine tatizo ni utamaduni mbaya uliojengeka wa kumwambia kiongozi habari ya kumfurahisha tu, na kuzuia yale mabaya. Lakini kufanya hivyo ni kumpotosha Rais. Pia ni kukosa ujasiri ambao kila waziri na mshauri wa Rais anatakiwa kuwa nao. Kama huko nyuma waliwahi kukosea, wakiiri hivyo. Na pale ambapo kosa lilikuwa la Rais mwenyewe na siyo washauri wake, kwa sababu na yeye pia ni binadamu, ni vyema akiri. Kwani "kujikosoa si kitendo cha kujidhoofisha bali ni kitendo cha kujiamini na kujiimarisha."

Wiki hii ma-DC wote wanakutana Kunduchi kwa semina elekezi nyingine. Wangefanya vyema kuzingatia ushauri huu wa Rais katika utendaji wao wa kila siku. Hata wakati wa semina, wangeanza kwa kusema ukweli tupu wa hali halisi wilayani, na kukosoa utendaji wa serikali na wao wenyewe. Daima, wangekumbuka ushauri wa Rais Kikwete aliotoa katika semina elekezi ya Ngurdoto:

"Wajibu wetu wa kwanza hapa ni kujua kwa uhakika wananchi wanataka nini? Wana shida gani? Wanakerwa na lipi baya tuliondoe? Kwa maoni yangu Watanzania wanapenda kuwa na Viongozi ambao wanawasikiliza, na wanaojali kushughulikia mambo yao (wananchi)."

Asasi za kiraia zinawajibikaje kifedha?

Na Daniel Luhamo*

Ilichapishwa 13 Machi 2007

Hivi karibuni baadhi ya watendaji wa serikali wamekuwa wakionyesha kutofurahishwa na mashirika ya kiraia yanaposisitiza uwazi na uwajibikaji serikalini. Changamoto ikitolewa, wao wanapenda kujibu: 'Kwani ninyi mashirika yasiyo ya kiserikali mnawajibika kwa nani? Na shughuli zenu ziko wazi? Hatujui mnapata pesa kutoka kwa nani na matumizi yake!'

Mtazamo kama huo unasikitisha, kwa sababu unakwepa ukweli wa changamoto serikalini na katika utoaji wa huduma za jamii. Udhaifu wa mahali pengine usitumiwe kuficha ukweli wa matatizo yako. Kuhoji sifa na uhalali wa mtu anayekukosoa ni mbinu inayotumika siku zote kukwepa hoja na uwajibikaji. Jambo la msingi sio tabia ya mtu anayehoji, ila uzito na ukweli wa hoja yake.

Kwa upande mwingine sisi mashirika ya kiraia tunaweza kufanya zaidi kuchochea uelewa, ubora wa hali ya juu na maadili ya utendaji kati yetu. Kamwe tusingoje viongozi wa serikali au wafadhili kutushinikiza kujirekebisha. La msingi siyo tu kuhusu pesa tunazotumia bali ni pamoja na uwajibikaji usio na shaka mbele ya jamii.

Mashirika ya kiraia yanawezaje kuimarisha uwajibikaji? Kwa uzoefu wetu, tunaweza kuanza na mambo sita yafuatayo:-

Kwanza, kuhakikisha shirika la kiraia lina sera ya fedha iliyoandikwa kwa ufasaha na lugha rahisi, na pia igawiwe kwa wafanyakazi wote, bodi ya shirika na mtu yeyote atakayependa kuiona. Sera hii itagusa mambo mengi, lakini haya mawili yafuatayo ni muhimu. i) Sera isisitize kuwa na watu wawili (pengine watatu itakuwa bora zaidi) kuidhinisha malipo. ii) Sera isisitize kuwa kila mapato na matumizi yawe na viambatanisho kamili na halisi. Hii inamaanisha kwamba mkuu wa shirika kwa mfano, hawezi kuidhinisha malipo peke yake na bila kutoa ushahidi wa kutosha ili kuhalalisha malipo hayo.

Pili, uwiano kati ya mpango, bajeti na matumizi halisi uwekwe kwa urahisi na uwe wa kueleweka. Umuhimu wake unaeleweka wazi, lakini utashangaa kuona kuwa ni mara nyingi imekuwa vigumu kulinganisha bajeti na mpango wa kazi. Pamoja na hayo, ripoti za matumizi halisi ikilinganishwa na bajeti ziandaliwe mara kwa mara.

Tatu, ni kuweka msisitizo wa pekee kwenye taratibu za ununuzi. Eneo hili ni moja ya maeneo yaliyozingirwa na rushwa serikalini na katika mashirika binafsi. Imefikia mahali 'dhana ya asilimia kumi' inaonekana kama ni jambo la kawaida katika ununuzi, na pale unaposita kuchukua wanakushangaa. Pamoja na utaratibu wa kuwa na ulinganishaji wa bei, kutangaza zabuni, na mengineyo ubadilishanaji wa taarifa pia vinaweza kusaidia. Mashirika yanaweza kuulizana kwa mfano: "mmetumia kiasi gani kununua kompyuta, au kuchapisha kijitabu". Pengine, ingetengenezwa tovuti ya wazi ambayo mashirika ya kiraia yangeitumia kuweka na kupata taarifa hizo. Makampuni na wafanyakazi wapewe namna ya kutoa taarifa kwa siri wanapoombwa rushwa au kuona upendeleo.

Nne, ni kukataa utamaduni wa kutoa na kupeana posho kwa kila kitu. Hivi ni kweli tunahitaji posho za vikao (siting

allowances) tunavyozungumzia mambo yanayotugusa au kutukera? Au kwa nini tudai, na kulipana posho kwa mafunzo yetu yanayotujengea uwezo? Pengine tujiulize hata viwango vyenyewe. Mtu anapewa posho ya usafiri shilingi 50,000 kwa mkutano unaofanyika kwenye mji ambao ni kituo chake cha kazi. Kwa tulio Dar es Salaam kiasi hicho kinaweza kukupeleka hadi Mwanza. Posho zinapoteza maana na umuhimu wa vikao na imefikia mahali watu wanachagua vikao vinavyolipa zaidi badala ya kuangalia mada inayotarajiwa kujadiliwa.

Ukitazama upande mwingine posho ndizo zinachangia kuleta matabaka na utofauti wa mapato sehemu za kazi kwa sababu wakubwa tu ndio wanaozipata zaidi. Hivi wahudumu wa ofisi na walinzi wa sehemu zetu za kazi ni lini walipata posho hizi? Nadhani kama tungeamua kutangaza hadharani posho tunazopata kwa mikutano na vikao mbalimbali nahisi wengi wetu tungetahayari.

Tano, ni kusisitiza hesabu za mashirika yasiyo ya kiserikali kukaguliwa kila mwaka na wakaguzi huru na wa nje wenye sifa zinazotambulika. Hii inaweza isiyahusu mashirika madogo, japo kwa mtazamo wangu yale yote yanayotumia zaidi ya shilingi milioni 20 kwa mwaka ni muhimu kufanya hivyo. Ikumbukwe kuwa ubora wa makampuni ya ukaguzi unatofautiana, hivyo mashirika yawe makini kutambua kampuni inayofaa. Aidha ripoti za wakaguzi ni vyema zikawa wazi kwa mtu yeyote anayehitaji kuziona.

Sita, bodi ya wakurugenzi inapaswa kutimiza majukumu yake kikamilifu. Mahali ambapo wakurugenzi hawahoji na kufuatilia shughuli za shirika, mambo huenda kombo. Mtendaji Mkuu wa shirika akitambua wakurugenzi wake wako makini siku zote atajitahidi kufanya kazi zake kwa ufanisi. Maana anajua asipofanya hivyo atawekwa kiti moto wakati wa vikao vya wakurugenzi. Kama hawezi kutimiza jukumu hili, heri asiwepo kwenye bodi.

Mwisho, shirika lisilo la kiserikali la kweli litakuwa ni lile linaloazimia na kupigania viwango vya juu vya uwajibikaji si kwa sababu serikali inataka hivyo au wafadhili wanalazimisha, bali ni kwa sababu wananchi wanastahili uwajibikaji wa kiwango hicho na si chini yake.

***Wachangiaji ni Nyanda Shuli na Richard Lucas.**

Muswada wa PCB: Tunapiga hatua au kurudi nyuma?

Na Hebron Mwakagenda
Ilichapishwa 20 Machi 2007

Ujio wa muswada wa PCB (Taasisi ya Kuzuia Rshwa) 2007 ni mapambano ya takribani miaka mitano. Wadau na PCB wamepiga kelele kwa muda mrefu kwamba hawana meno hivyo hawawezi kung'ata na kupambana na rushwa ipasavyo. Badala yake tunaendelea kukamata wanaotoa na kupokea hongo badala ya rushwa ambayo wenzetu wa Kenya wanaiita ufisadi.

Hivyo basi inafurahisha kuona Serikali imeandaa na kutoa muswada wa PCB kwa umma. Pamoja na uwezekano kwamba hatua hii imechukuliwa kwa shinikizo kubwa la wafadhili, suala nyeti hapa ni je muswada unazingatia maslahi ya watanzania ? Je matatizo yaliyoonekana wazi na sheria ya sasa hivi yametatuliwa ?

Muswada umekusudiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi ujao. Kama watanzania makini, tunawajibu wa kuuchambua kwa makini na kutoa hoja zetu.

Tumepitia muswada na tumekuta, pamoja na maeneo mazuri, bado kuna mapungufu makubwa na kama yatapitishwa bungeni kama yalivyo basi vita dhidi ya rushwa mambo yatakuwa ni yaleyale kama ilivyo sasa, na chombo cha PCB kitakosa meno ya kufanya kazi yake.

Nitachambua madhaifu na kupendekeza mbadala kama yalivyojadiliwa na kuchambuliwa na mtandao wa mashirika ya kiraia wa kupambana na rushwa hapa Tanzania (Civil Anti-Corruption Initiative-CACI). Madhaifu yako mengi lakini nitajitahidi kujielekeza kwenye maeneo matano makuu ili kulenga na kuweka mwelekeo wa hoja za msingi za CACI.

Kwanza, maana ya rushwa: Katika muswada unaopendekezwa ili kuimarisha utendaji wa PCB ambayo sasa inakuwa PCCB hakuna tafsiri thabiti ya rushwa inayoainisha rushwa ni nini na mipaka. Tunapendekeza kuwa tuwe na tafsiri pana ambayo itaainisha kama inavyotafsiriwa na umoja wa mataifa (UN) na umoja wa nchi huru za kiafrika (AU).

Pili, uhuru wa bodi: Muswada unapendekeza kuwe na bodi ambayo itasimamia shughuli za PCB ambayo wajumbe watakuwa Katibu Mkuu Kiongozi (Mwenyekiti), Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Mkuu wa Usalama wa Taifa, Mwanasheria Mkuu (AG), na wajumbe wawili mmoja kutoka sekta binafsi na mmoja kutoka kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali.

Bodi ya aina hii inaweza kushindwa kuwa bodi huru. Tunapendekeza kusiwe na bodi na badala yake PCCB iwe kama ilivyo sasa. Isipokuwa PCCB iripoti bungeni moja kwa moja kila mwaka. Kama kutakuwa na ulazima wa kuwepo bodi mambo mawili yafanyike. Moja tuige wenzetu wa Korea Kusini ambayo wajumbe wawili wanateuliwa na Rais, wawili na Bunge na wawili wateuliwe na Mahakama. Katika Mahakama Mmoja ateuliwe na Jaji Mkuu na mwingine na Mwanasheria Mkuu na wengine wawili wa Sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya kiserikali waendelee kubaki na wateuliwe na mashirika yao kitaifa.

Pia jukumu la kushauri kuhusu mambo ya rushwa ni vizuri liondolewe kwenye majukumu ya bodi. Jukumu hili waachiwe wataalamu na watendaji wa kila siku vinginevyo bodi itaingilia utendaji wa PCCB na hasa itakapotokea mgongano wa kimaslahi.

Tatu, uhuru wa PCB: Kwa muda mrefu tumepigania taasisi ya kuzuia rushwa iwe huru ili iweze kufanya kazi zake ipasavyo. Tunapendekeza mambo sita ambayo yataihakikishia uhuru wake. (i) PCCB ianzishwe kikatiba, (ii) isiwe chini ya Rais iwe chombo huru kama ilivyo Tume ya Haki za Binaadamu na utawala Bora, (iii) Itoe taarifa zake bungeni, (iv) Fedha zake zitoke kwenye mfuko maalum (Consolidated fund), (v) Ipewe pia jukumu la kuendesha mashitaka ambalo tunashauri liondolewe kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) na Mwanasheria Mkuu (AG) na (vi) Kinga ya maofisa wa PCCB Mkurugenzi Mkuu akiteuliwa na Rais asiondolewe kirahisi mpaka apigiwe kura ya kutokuwa na imani na bunge.

Nne, adhabu iliyopendekezwa haitoshi: Inavyoonyesha muswada unakusudia kupambana na hongo na sio rushwa au ufisadi. Kwa sababu inapendekezwa kuwa mtu akipatikana na hatia hukumu yake itakuwa kifungo kisichozidi miaka miwili au faini ya shilingi za Kitanzania laki tano (500,000). Ukisoma sheria ya Anti-Money Laundering adhabu ni kifungo cha miaka kumi au faini ya shilingi za kitanzania milioni kumi (10,000,000). Tunadhani kosa la rushwa na hasa rushwa kubwa (grand corruption) huleta athari kubwa kwa jamii. Hivyo tunapendekeza tuchukue adhabu iliyoko kwenye sheria ya anti-money laundry hii itafanya watu waogope na tunaenda mbali zaidi kupendekeza kuwa anayepatikana na kosa afilisiwe mali zake zote zilizopatikana kwa njia ya rushwa na pia jamii iliyoathirika na kitendo hicho ifidiwe.

Tano, kulinda watoa taarifa: Watoa taarifa (whistle blowers) ni watu muhimu katika vita dhidi ya rushwa. Aidha tunapendekeza itungwe sheria peke yake inayohusu watoa taarifa ambayo itakuwa imejitosheleza na kuangalia watoa taarifa kwa upana wake. Hii ni pamoja na kulindwa na kufidiwa pale ambapo watapata madhara kutokana na kitendo chao cha kutoa taarifa kwa hiyari kama raia wema.

Kama mambo haya matano tuliyoyaorodhesha hapa juu yatapewa uzito unaostahili na kuingizwa kwenye muswada husika, tutakuwa na PCCB unaotufaa. Haitakuwa na kisingizio chochote na wananchi tutarajiwe kuwapa ushirikiano tukijua kuwa tumewapa kila aina ya msaada na nyenzo wanazohitaji kutimiza wajibu wao.

Sera bila utafiti kweli tutafika?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 15 Mei 2007

Tunawezaje kutoa maamuzi ya tatizo fulani bila kutafiti na kulijua tatizo kwa kina? Tunapata nini kuacha nyuma tafiti na kukimbilia kuamua au kutunga sera? Inawezekana maswali haya ndio yaliyozaa usemi usemao "bila tafiti huna haki ya kulisemea jambo" (no reseach no right to speak).

Sera na tafiti ni maneno yanayotumiwa sana na viongozi, wanasiasa, na hata wasomi. Pengine ndio maana yamekuwa ni maneno maarufu katika jamii japo kwa mtu wa kawaida ni ngumu kupata moja kwa moja maana za maneno haya.

Sera ni program ya hatua kwa vitendo zinazopangwa kwa ajili ya kulinda na kutambua maamuzi ya sasa na ya baadae ili kufanikisha lengo lililokusudiwa. Na utafiti ni uchunguzi makini wa kubaini chanzo halisi cha tatizo, ukubwa wa tatizo, mazingira ya tatizo na hatimaye kupendekeza njia za kutatua tatizo hilo. Mara nyingi matokeo ya tafiti yanapofanyiwa kazi ndio huzaa sera makini ambazo zinayaelezea matatizo na kuyawekea program yenye lengo la kuyatatua.

Bila tafiti kuna uwezekano mkubwa wa sera au program kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Tafiti ndio zinazochimbua ukweli wa suala/tatizo linaloikabili jamii, tafiti ndio zinatambulisha chanzo cha tatizo, ukubwa wa tatizo, na pia tafiti zinaibua mbinu tawanyishi za kushughulikia tatizo hilo. Bila tafiti ni sawa na kuanza safari bila kujua unapoelekea.

Inawezekana program nyingi za utatuzi wa matatizo katika jamii zimeshindwa au kuwa zinasuasua kwa kutotanguliwa na tafiti zilizolenga kuibua njia bora za kulitatua. Chukua mfano wa tatizo la Wamachinga waliohamishwa toka Jiji la Dar es Salaam ambalo hadi leo bado linasikika. Pengine hili linatokana na kukosa utafiti kwanza wa kujua idadi ya machinga wako wangapi, na hivyo watahitaji eneo kubwa kiasi gain? Na je watapata soko wakiwa eneo lipi, huduma muhimu kama vyoo na maji vitapatikana? Haya inawezekana yametokea kwa sababu hakukuwa na tafiti kabla ya kutolea maamuzi na pengine ndio maana hadi leo tatizo linaendelea.

Hivi majuzi pia tulishuhudia program ya mikopo kwa wajasiriamali masikini, ilivyoibua mkanganyiko mkubwa. Badala ya kuleta neema kwa baadhi ya walengwa ikawa lawama na fedheha. Kwani baadhi yao licha ya kuhangaika huku na kule hatimaye waliishia kuja kuambiwa kuwa hawakustahili kupewa mikopo hii au kuwa imeisha, n.k. Inawezekana utata usingekuwepo kama utafiti ungetangulia kwanza ikajulikana tabaka halisi la walengwa, idadi yao, sifa za walengwa na kiwango cha pesa kilichopo. Inaelekea hili halikuwepo na kuna hatari mwisho zoezi litaishia kuwapatia mikopo watu wenye sifa za kupata mikopo benki na sio wajasiriamali masikini waliokusudiwa.

Aidha, hivi sasa kuna hili sakata la wanafunzi wa Chuo Kikuu kulipa asilimia 40 ya ghrama ya masomo yao lililofikia hatua ya kulazimika kuwafukuza baadhi ya wanafunzi.. Inawezekana kusingekuwa na mgogoro huo kama kungekuwa na tafiti kwanza kuhusu hali ya wanafunzi, taratibu

zinazoweza kutekelezeka na taratibu zinazotumika katika nchi zingine. Kwa mfano pengine ingefaa zaidi kuwasomesha 'bure' kwa sasa na kudai fedha kwa waajiri baadaye. Badala yake hali ya sasa hivi inatisha kwa sababu pande zote zinaonekana kutoelewa upande mwingine. Kwa hali ilivyosasa kuna hatari dhahiri kuwa baadhi ya wanafunzi kutoka familia masikini kweli watashindwa kurudi au kusoma vyuo vikuu.

Makamu wa Rais, alipokuwa akifungua Warsha ya Tafiti tarehe 2 Mei 2007 huko White Sands Hotel, alisisitiza kuwa serikali inatambua umuhimu wa tafiti katika kuleta maendeleo ya taifa. Hata hivyo alikiri changamoto zinazoikabili sekta hiyo muhimu. Hili lilikuwa dhahiri pia kwa wadau wa tafiti wengi waliohudhuria semina hiyo muhimu.

Msingi wa tatizo ni nini? Je, ingesaidia kuwa na bajeti au mfuko maalum wa pesa za tafiti? Fedha hizi zingesaidia kuchambua matatizo yanayoibuka mara kwa mara? Au je kufanya hivyo ingepoteza pesa zaidi kwa sababu tafiti zingekuwa zinafanyika mbali na matatizo na utendaji wa sera?

Kutotumika kwa tafiti ambazo tayari zimeshafanywa ni changamoto kubwa. Ripoti nyingi nzuri 'zinakaa kwenye mashelfu' na kusomwa na watu wachache tu. Mara nyingi inasemekana watoa maamuzi na watunga sera hushindwa kutumia tafiti ili ziwaongoze kutunga sera sahihi. Maeneo haya yanahitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha utendaji na kufikia malengo kwa ufanisi zaidi. Suala ni, je viongozi wetu watafanya hivyo?

Pengine serikali ingejenga utamaduni wa kutambua viongozi wanaotumia tafiti, na kuwawajibisha wale wanaofanya maamuzi bila tafiti. Lakini kufanya hivyo kunahitajika kuwapo kwa viongozi kuanzia ngazi ya taifa hadi chini kabisa wanaoheshimu na kuthamini kazi yenye msingi wa utafiti. Bila hivyo tafiti zitaendelea kubaki kwenye mashelfu.

Nchi zilizoendelea duniani zilifanya juhudi makini kuimarisha tafiti, kuheshimu tafiti, kutumia matokeo ya tafiti katika kupanga sera na program za maendeleo, na kukosoa utendaji. Sera au programu bila kutanguliwa na utafiti ni kuishi maisha ya kubahatisha, ya alinacha. Matokeo yake ndiyo tunabaki masikini licha ya kuwa na rasilimali lukuki. Unawezaje kunywa dawa bila kujua ugonjwa wako?

Misitu yetu inamnufaisha nani?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 5 Juni 2007

"Serikali inapoteza karibu shilingi bilioni 58 mapato yatokanayo na misitu hasa kwenye uvunaji na uuzaji wa mbao na magogo nje ya nchi…mapato haya ya serikali yanayopotea kila mwaka kutokana na mavuno ya misitu ni karibu asilimia 96 ya mapato yanayopaswa kukusanywa. Na hivyo serikali huambulia asilimia 4 tu ya mapato.." (Ripoti ya TRAFFIC ukurasa wa 4)

Hasara ya mabilioni haya kwa Mujibu wa mkurugenzi wa TRAFFIC yangeweza kununua vyandarua karibu milioni 11 na kujenga vyumba vya madarasa karibu 5,000 pamoja na kusaidia uboreshaji wa huduma nyingi za jamii.

Hii ni sehemu ndogo tu ya ripoti ya utafiti uliofanywa kwa niaba ya Serikali na shirika la ufuatiliaji wa biashara ya rasilimali misitu na Wanyamapori lijulikalo kama TRAFFIC. Utafiti huu ulifanyika kusini mwa Tanzania na kuchapishwa mapema mwaka huu. Serikali na TRAFFIC wanapaswa kupongezwa, kwa sababu utafiti uliofanyika ni thabiti na unatupa mwanga.

Utafiti huo umegundua Tanzania inapoteza asilimia 96, sawa na shilingi bilioni 58 kila mwaka toka mazao ya misitu. Na hii inaifanya sekta ya misitu kuwa haina faida kwa watanzania wengi. Sababu za hasara hii kubwa zimebainishwa na ripoti kama ifutavyo:

Moja, rushwa kubwa na ndogo ndizo zinaitafuna sekta ya misitu. Ukurasa wa 109 wa ripoti unaonesha kuna rushwa kuanzia ngazi ya vijiji hadi ngazi za juu serikalini. Rushwa hiyo inafanywa kwa kutoa hongo, kukwepa kodi, upendeleo kwa ndugu au jamaa. Kulindana na kuhalalisha uvunaji haramu kwenye maeneo yasiyoruhusiwa pia kumebainishwa.

Rushwa inayotisha zaidi iko kwenye ugongaji wa mihuri kwenye magogo na usafirishaji wa magogo nje ya nchi. Mfano ukurasa wa 115-116 wa ripoti hiyo unaonesha kuna asilimia 78 ya rushwa kwenye ugongaji wa mihuri na asilimia 62 ya rushwa katika usafirishaji wa mbao na magogo nje ya nchi.

Mwezi Julai mwaka 2004, waziri mwenye dhamana ya misitu alitembelea Bandari ya Dar es Salaam na kugundua makontena 187 yamejaa mbao na magogo yaliyopatikana kwa njia haramu. Vivyo hivyo ukaguzi wilaya za Pwani ulibaini magogo yenye thamani ya shilingi milioni 382.6 yalivunwa kwa njia haramu.

Pili, matumizi ya nyaraka bandia, vibali bandia na mihuri bandia, ni tatizo kubwa na linachangia hasara hii. Ukurasa wa 107 umeweka bayana karibu asilimia 60 ya mavuno ya misitu yanayosafirishwa nje yana nyaraka bandia, vibali bandia, yana mihuri bandia. Na pia yanasafirishwa nje ya nchi kupitia njia haramu. Na hivyo kukwepesha mapato makubwa kwa serikali.

Tatu, utafiti umeonesha karibu asilimia 80 ya makampuni yanayojihusisha na uvunaji wa mbao na magogo yanamilikiwa na viongozi wakubwa serikalini au kuhusihwa nao ki-ubia, kimaslahi, au katika ujumbe wa bodi na kuwa washika dau kwa namna moja ama nyingine. Kwa mujibu wa aripoti hiyo, kati ya makampuni 35 yaliyokuwa yakifanya biashara ya mbao na magogo 28

yalikuwa yakimilikiwa na baadhi wa viongozi wa Serikali.

Hali hii imetoa mwanya mkubwa wa rushwa, upendeleo, ukwepaji kodi na uvunaji hovyo wa misitu katika maeneo yasiyoruhusiwa. Ripoti hii ya Serikali imebainisha haya ukurasa wa 9 na 10, na kuainishwa vizuri katika jedwali ukurasa wa 126.

Nne, viongozi wa serikali za vijiji na wilaya wanajihusisha na biashara ya mbao na magogo moja kwa moja. Ripoti imebaini karibu asilimia 60 ya viongozi wa vijiji wanamiliki wingi wa mbao na magogo nyumbani kwao.

Hii imechangia ukusanyaji hafifu wa mapato, ukwepaji kodi za mapato na kodi za kuhodhi misitu. Hali hii pia inachangia kuficha taarifa kwa wananchi juu ya thamani ya misitu na mapato yatokanayo na misitu; na hivyo kuwafanya wananchi kukosa taarifa na kushindwa kufuatilia. Ukweli huu uliambatana na picha halisi zilizopigwa kwenye baadhi ya kaya za viongozi wa vijiji zikionesha magogo na mbao (ukurasa wa 125).

Tano, udhaifu mkubwa wa utendaji wa viongozi wa sekta hii pengine umechangia kuhalalisha uvunaji haramu. Hakuna ufuatiliaji mzuri, sheria kali wala nidhamu ya utendaji. Hii imefanya sekta ya misitu iwe kama imetelekezwa na haina mwenyewe, na hivyo kuacha uvunaji holela ukiendeshwa.

Suala hili linaaambatana na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu thamani ya misitu na faida zake kwa maendeleo yao. Uelewa mdogo na uhaba wa taarifa umewafanya wananchi wakose uwezo wa kufuatilia na kuhoji mapato na matumizi ya mazao ya misitu. Ripoti imebaini kuwa wananchi wengi hawajui habari za mapato ya mbao na magogo na pengine katika ofisi za vijiji na kata taarifa hizo hazipo kabisa. Je ni lini Serikali itadhibiti hali hii?

Mwisho, nirejee tena kuipongeza Serikali kwa kukubali kufanya utafiti huu muhimu. Utafiti huu ni changamoto kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Katibu Mkuu wake mpya aliyeteuliwa hivi karibuni na Rais, anaweza kufuatilia na kudhibiti hali hii, ili kuokoa misitu yetu na kuliongezea taifa mapato makubwa. Kufanya tafiti thabiti ni hatua ya kwanza kutatua tatizo; sasa wananchi wanahitaji vitendo vya uwajibikaji.

Mfuko wa majimbo utainufaisha jamii?

Na Rose Mushi
Ilichapishwa 26 Juni 2007

Kuna uwezekano wa karibu bilioni 200 kutengwa kwa ajili ya mfuko wa maendeleo wa majimbo. Fedha hizi ni kwa ajiri ya shughuli za maendeleo majimboni. Chini ya mpango huo, kila Mbunge atagawiwa fungu lake la fedha ili akazitumie katika jimbo lake kwa lengo la`kuwaletea` maendeleo wananchi wake.

Kiasi hiki cha fedha kilichopangwa kutolewa ni kikubwa sana; Kwani ni sawa na asilimia nne ya bajeti nzima ya taifa na ni mara tatu ya kiasi kilichotengwa kwa serikali za mitaa kwa ajili ya maendeleo.

Kimsingi malengo ya Mfuko huu ni mazuri na yanafaa kupongezwa. Lakini swali lililopo ni je, utekelezaji wake kweli utawanufaisha wananchi?

Uzoefu wa nchi za Kenya na Uganda katika kuendesha mifuko ya aina hii unaonesha kuwa tahadhari kubwa inahitajika ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza. Mifuko kama hii ina mapungufu mengi. Baadhi yake ni kama yafuatayo:

Kwanza, dhana ya Mfuko huu inapingana na Katiba ya nchi juu ya mgawanyo wa madaraka katika dola. Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Kazi yao kubwa ni kupeleka matatizo ya wananchi serikalini ili yafanyiwe kazi, kutunga sheria na kujadili na kuidhinisha bajeti. Pia kuithinisha makadirio ya mapato na matumizi ya serikali na kusimamia serikali katika kutekeleza mipango ya maendeleo.

Wabunge ndio jicho la uwajibikaji wa mawaziri na watendaji Serikalini. Badala ya majukumu yao haya. Mfuko huu unawageuza wabunge kuwa watoa huduma badala ya kuwa wasimamizi au waangalizi. Hali hii inaweza kufanya uendeshaji wa serikali za mitaa kuwa mgumu zaidi na kusababisha kuweko kwa mazingira ya rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma.

Pili, Mfuko huu ni kikwazo kwa maendeleo ya demokrasia nchini kwani si tu hautusadii kujenga uelewa juu ya demokrasia ya uwakilishi nchini bali pia unaipotosha. Lengo la majimbo ya uchaguzi na muundo mzima wa uwakilishi si kwa ajili ya utendaji kama zilivyo Halmashauri na Manispaa.

Ndani ya Mfuko wa majimbo ushindani wa kisiasa utakufa. Kwani mtu mwingine asiyekuwa na hayo mamilioni, aslani hawezi kwenda kwenye jimbo kugombea na akatarajia kushinda. Kuna hatari kubwa kuwa huenda ukatoa mianya ya rushwa na ushindani wa kisiasa usiokuwa wa haki. Pia upo uwezekano kuwa pesa hizi zikatumika kuwahonga wananchi na hivyo kupatikana kwa viongozi waliochaguliwa pasipo haki kutendeka.

Kutokana na umaskini uliokithiri miongoni mwa wapiga kura, na uelewa mdogo wa haki na uhuru wao wa kidemokrasia wa kuchagua kiongozi anayeweza kuleta maendeleo endelevu, wengi wao wamekuwa wakitoa kura kwa mtu anayewapa vizawadi vidogovidogo kanga, pombe au chakula (takrima).

Tatu, udhibiti wa matumizi ya fedha hizo utakuwa mgumu sana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mbunge hana chombo cha uendeshaji wa shughuli za maendeleo. Halmashauri na serikali za mitaa ndivyo vyombo vya utekelezaji wa miradi ya

maendeleo na vimeundwa kwa madhumuni hayo.Vina uwezo wa kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo na kudhibiti matumizi ya fedha ipasavyo.

Nne, dhana nzima ya Mfuko huu haiendani na Sera ya kuimarisha Serikali za mitaa ya mwaka 1998 ambayo inatutaka kuviimarisha vyombo vya utendaji ambavyo ni Halmashauri na Manispaa kwa kuvipa madaraka na nyenzo za kuleta maendeleo na siyo majimbo ya uchaguzi.

Swali tunalopaswa kujiuliza ni je, kama pesa watapewa wabunge halmashauri zitatekelezaje wajibu wa kuleta maendeleo kwa wananchi? Aidha ni dhahiri kuwa wabunge watatumia muda mwingi kutekeleza miradi itakayotokana na fedha za Mfuko huu badala ya kufanya kazi ya kusimamia fedha za Halmashauri. Na hii itafanya utendaji wa halmasahauri ulegelege kwa kukosa usimamizi wao.

Tano, kama ilivyogusiwa hapo juu, Mfuko huu utachochea rushwa hususani katika kipindi cha uchaguzi. Je, Mfuko huu hautakuwa neema kwa watoa rushwa na wala rushwa majimboni? Wabunge hawatayatumia mamilioni ya fedha hizo kuwaadhibu wapinzani na kuwazawadia wafuasi au kutumia pesa nyingi kabla ya uchaguzi ili kuwaghilibu wapiga kura?

Kwa kifupi Mfuko wa Majimbo ni dhana tata inayohitaji mjadala mpana wa jamii ili kubainisha kama kweli inauhitaji na iamue kama huu ni mfumo sahihi kwa maendeleo yao. Jamii inabidi kuchukua tahadhari zote ili tusije tukajikuta katika matatizo kama yaliyowasibu wenzetu wakenya na uganda.

Ni vyema ikaeleweka kuwa kidemokrasia serikali za mitaa ni eneo muhimu. Kwani fedha zinazotumika katika serikali za mitaa mara nyingi hutumika kutoa huduma kwa umma kwa kuzingatia viapaumbele vya jamii husika.Itakuwa kosa kubwa mfumo huu ukivurugwa.

Ingefaa zaidi kuona watendaji katika halmashauri za wilaya na manispaa wakijengewa uwezo wa mambo ya kifedha na usimamizi wa miradi ili kuondoa kasoro ndogondogo ambazo zimekuwa zikijitokeza wakati wa kusimamia fedha na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Pengine ingefaa zaidi kuwashirikisha wananchi katika kuamua juu ya suala hili. Kwa nini wananchi wasiulizwe kwanza? Bila hivyo itakuwa ni kuwaburuza kwenye mifumo hasi inayodidimiza maendeleo na demokrasia yao.

Je kudai uwakilishi 50/50 Bungeni ni sawa?

Na Agnes Mangweha
Ilichapishwa 3 Julai 2007

Wanawake wengi sasa wako bungeni kwa tiketi ya viti maalum. Je majukumu yao ni yapi? Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la 2 inasema "Mbunge ni mtu aliyechaguliwa na watu kuwawakilisha bungeni". Tunao wabunge wa kuteuliwa na wa viti maalum.

Katika wabunge wanawake 97 ambao ni sawa na asilimia 30.4 ya wabunge wote, 75 ni wa viti maalum; 22 tu ndio wa kuchaguliwa. Je wabunge hawa wa kuteuliwa wanamuwakilisha nani? Na, je. uwakilishi huu ni sahihi?

Hivi karibuni nimeona bango linalodai uwakilishi wa asilimia 50 kwa wanawake katika kila ngazi za uongozi. Hoja hii ndiyo imenisukuma kuandika makala hii. Hapa silengi kuupinga mfumo huu, bali ni kuangalia kwa jicho pevu umhimu wa madai haya.

Licha ya madai haya, bado kuna wasiwasi mkubwa kuhusu utendaji au uwakilishi wa hao wabunge. Kuna masuala mengi sana ya akina mama na jamii kwa ujumla yanayohitaji hasa sauti za wanawake kuyatetea na kuyapigania. Lakini sauti hizo hazisikiki kabisa bungeni. Je kuna umuhimu gani wa mbunge kuwa bungeni huku hawafanyi lolote?

Wanawake wanapomchagua mbunge mwanamke mwenzao, wanatarajia kuwa atawasemea mambo yao mengi zaidi. Ili kuridhisha matarajio haya mbunge huyu anapaswa kudhihirisha uwezo wake wa uwakilishi kuliko wabunge wanaume Mara nyingi masuala ya wanawake hayapewi umuhimu. Je hawa wabunge wa kuteuliwa kweli wanaweza kuwa wametuonesha athari chanya zinazochacharikia mambo ya akina mama?

Historia ya Viti maalum bungeni ni ya siku nyingi. Viti hivi vilianzishwa kwa ajili ya kupaza sauti bungeni za makundi maalumu kama vile walemavu, watoto n.k. Lengo kuu lilikuwa ni kudumisha demokrasi na kuendeleza maslahi ya Taifa na siyo kuleta usawa wa jinsia bungeni.

Ndiyo maana wabunge hawa wakajulikana kama wabunge wa taifa wanaowakilisha maslahi ya taifa. Hata hivyo, maslahi ya taifa haya hayakubainishwa kinagaubaga. Kutokana na kuweka kipaumbele maslahi ya taifa wabunge hao walidiriki hata kukataa kuitwa wabunge wa wanawake; bali wabunge wa taifa.

Napata wasiwasi na wabunge hawa kama kweli wanasukumwa na uzalendo wa kuwakilisha wanawake kwa maslahi ya taifa au wana malengo binafsi. Kati ya wabunge 75 ni wachache sana wanaosikika wakipigania masuala yanayotuathiri wanawake.

Ukiondoa masuala machache mathalani kupigania mabadiliko katika sheria kama vile wasichana kupewa nafasi zaidi elimu ya juu , sheria ya makosa ya kujamiiana n.k., mambo mengi yanayomkera mwanamke bado hayana mtetezi licha ya kuwa na wingi wa uwakilishi bungeni. Masuala hayo ni kama yafuatayo:-

Moja, vifo vya uzazi kwa mama na mtoto. Jambo hili bado ni tishio kwa akina mama hususani vijijini. Jamii ilitegemea sauti za wabunge wanawake zisikike zaidi kupigania harakati za kuliondoa tatizo hili ili

kulinusuru taifa. Lakini licha ya kujua ukubwa wa taizo hili wabunge hawa wako kimya.. Kelele zao kwa watunga sera, taasisi za kifedha na wadau wa maendeleo zingewafanya walitambue tatizo na kuchukua hatua za haraka kuwanusuru akina mama na watoto.

Mbili, Janga la ukimwi kwa akina mama ni tishio kubwa, hasa vijijini. Tulitarajia kuwa wabunge wanawake wangekuwa mstari wa mbele kwenda huko vijijini si kutoa mafunzo ya kujikinga na ukimwi tu, bali pia kuwafundisha jinsi ya kutoa lishe bora kwa wagonjwa katika familia zao.Lakini hilo nalo pia hatujaliona.

Tatu, Umaskini uliokithiri. Wanawake wengi ni masikini na hawana fursa za kujiendeleza. Ni wanawake wangapi vijijini wanaojua kuwa kuna mikopo inayotolewa na serikali na jinsi gani wanaweza kuipata? Hii ingekuwa kazi ya wabunge wanawake kuwasaidia wenzao kupata mwanga huu. Kwa nini wabunge hawalioni hili?

Tulitarajia ongezeko la wabunge wanawake lingekuwa na athari chanya kwa wanawake. Wabunge wangeweza kutoa elimu kwa wanawake vijijini. Wangeweza kwa mfano kuhamasisha miradi ya maendeleo, kuwasaidia kuomba mikopo kwenye mabenki kwa kuwaelekeza taratibu zilizopo. Lakini hayo watafanya saa ngapi wote wamengángánia mijini kwa maslahi yao binafsi?

Nne, Ukataji ovyo wa misitu.Kuni na mkaa bado ndizo nishati kuu kwa kupikia lakini zinatusababishia jangwa nchini. Akina mama wanahangaika sana kupata nishati ya hii kupikia. Wabunge hawa walitarajiwa kupigia kelele tatizo hili ili ipatikane teknologia nafuu ya kuwanusuru akina mama na taifa

Tano, Mimba kwa wasichana na utoro shuleni. Tulitarajia wabunge wanawake wawe mstari wa mbele kupinga hili. Cha kushangaza wako kimya. Badala yake kazi hii inaonekana ameachiwa Waziri Mkuu na Mama Kikwete. Je kama hili si jukumu lenu wabunge wanawake mko bungeni kufanya nini? Na bado mnataka uwakilishi wa 50 kwa 50 ili iweje?

Nadhani, wabunge wanawake wangejitathimini kwanza utendaji wao bungeni na kwa jamii kabla ya kudai zaidi.Usawa wa jinsia bungeni utakuwa na maana tu pale kila mbunge anapotimiza wajibu wake.

La sivyo warudi kugombea majimboni ili wananchi waamue. Haina maana kuwa na watu bungeni wanaotumia mamilioni fedha za watanzania kwa kukaa tu. Nani mkombozi wa wanawake kama siyo wao?

Sheria ya kulinda watoto inamsubiri nani?

Na James Marenga
Ilichapishwa 24 Aprili 2007

Mtandao wa asasi zisizokuwa za kiserikali zinazofanya kazi na au kwa niaba ya watoto chini Tanzania (NNOC), uliwasilisha tamko kwa Mhe. Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kumkumbusha umuhimu wa kutungwa kwa sheria mama inayolinda haki za watoto hapa nchini. Mtandao huo na asasi hizo zilifanya hivyo baada ya kuona hakuna maendeleo ya maana ya kutunga sheria ya kuwalinda watoto.

Tanzania ni nchi pekee kwenye Jumuia ya Afrika Mashariki ambayo haijatunga sheria moja inayolinda haki za mtoto, Kenya na Uganda tayari wana sheria hiyo. Nchi ya Kenya imetunga sheria hiyo kwa kutumia taarifa iliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria nchini (TUMESHERIA), baada ya kufanya tafiti mabalimbali zinazohusiana na haki za mtoto.

Mnamo mwaka 1989 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (*UN General Assembly*) lilipitisha kwa kauli moja Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto (*UN Convention on the Rights of the Child, 1989*). Tanzania ilisaini Mkataba huu Mnamo mwaka 1990, na kuuridhia mnamo mwaka 1991.

Mnamo mwaka 1990, Umoja wa Nchi Huru za Afrika (*Organization of African Unity*) lilipitisha Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto (*African Charter on the Rights and Welfare of the Child, 1990*).

Tanzania ilisaini na kuuridhia Mkataba huu katika kikao cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania cha Februari 2003. Tanzania iliridhia mikataba yote hii miwili bila kuweka masharti ya utekelezaji wake hapa nchini (*ratification without reservations*).

Hivyo, kwa kusaini na kuridhia mikataba hiyo hapo juu (bila masharti ya utekelezaji), Tanzania ni mwanachama wa mikataba hiyo hapo juu; na kwa hali hiyo, inawajibika kuhakikisha kwamba vipengele vyote muhimu vya mikataba hii miwili vinatekelezwa hapa nchini.

Kwa mujibu wa mikataba hii, kila nchi mwanachama katika mikataba hiyo inapaswa kuhakikisha kwamba vipengele vyote vya mikataba hii vinatekelezwa katika nchi husika; ambapo utekelezaji huo ni kupitia Sheria na Sera za nchi husika.

Aidha, kama Sheria au Sera za nchi husika haviendani (au vinapingana) na vipengele vya mikataba hii, basi sheria na sera hizo zinapaswa kufanyiwa marekebisho ili vioane au kukubaliana na matakwa ya mikataba hii.

Hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijafanya marekebisho yoyote katika Sheria zake zinazogusa haki za watoto nchini, licha ya kwamba nyingi ya sheria hizo zinaathiri utetezi na ulinzi wa haki za watoto nchini.

Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukishuhudia jinsi ambavyo watoto katika makundi mbalimbali wanavyonyimwa haki zao kwenye maeneo mbalimbali hasa yale ya kisheria kwa kutumbukizwa kwenye migogoro ambayo kimsingi wasingepaswa kuwa humo.

Mnamo mwezi Juni mwaka 2006, Kamati ya kusimamia Utekelezaji wa Mkataba wa

Umoja wa Matiafa juu ya Haki za Mtoto ilitoa Ripoti yake ya mwisho juu ya hali ya haki za watoto nchin. Ripoti hiyo ilibainisha kuwa bado kuna sheria nyingi zinazogusa haki za mtoto hapa nchini ambazo hazijafutwa wala kufanyiwa marekebisho tangu Mkataba huo upitishwe na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1989!

Baadhi ya sheria ambazo ni kandamizi kwa haki za mtoto ni pamoja na ile ya Ndoa hasa kuhusu umri wa ndoa kwa wasichana, Sheria ya Watoto na Vijana kuhusiana na watoto kutenda makosa ya jinai, Sheria ya Elimu juu ya viboko shuleni na Sheria ya Mirathi.

Watoto wengi wanaendelea kupata matatizo mbalimbali yanayoathiri makuzi yao na wala hakuna anayejali kana kwamba hakuna aliyepita kwenye umri wa utoto. Watoto wameendelea kuolewa wakiwa na umri mdogo, wamekatishwa masomo yao, unyanyasaji wa kijinsia, kukosa matibabu ya uhakika na kuhusishwa kwenye biashara haramu za ngono na kutumikishwa.

Serikali kupitia mkutano wa wadau uliondaliwa na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, mwezi Novemba mwaka 2001, uliofanyika mjini Morogoro, iliwahi kutoa ahadi ya kutunga sheria mpya ya kutetea haki za watoto ifikapo Julai 2007. Kwenye mkutano huo Serikali iliahidi kwamba muswada wa sheria hiyo ungewasilishwa kwa kusomwa kwa mara ya kwanza katika kikao cha Bunge la Jamhuri cha Februari 2002. Pamoja na kutoa ahadi hizo, jambo la kushangaza ni kuwa, hadi leo hii Serikali haijawasilisha bungeni muswada wowote kuhusiana na haki za watoto.

Waziri Simba anahitaji kutoa tamko ni lini mchakato wa White Paper utanza ili kukusanya maoni ya wananchi kuhusiana na sheria mpya ya watoto. Waziri pia ahakikishe kuwa watoto wanashirikishwa kikamilifu kwenye mchakato huo. Sisi wanaharakati tunamhakikishia Waziri ushirikiano wa dhati kuhakikisha kuwa sheria mama ya watoto inatungwa kuendeleza haki za watoto wa Tanzania. Penye nia pana njia.

Tumepata dawa ya foleni za magari?

Na Richard Lucas
Ilichapishwa 29 Mei 2007

Foleni za magari jijini Dar es Salaam bado ni kero. Kwa wastani watu wengi hutumia muda wa saa 3 kila siku kwenda kazini na kurudi. Muda huu mwingi unapotea bila manufaa yeyote, magari yanachakaa na pia mazingira yanachafuliwa na hewa chafu inayotokana na injini za magari haya.

Tatizo la foleni limeanza kuchukuliwa hatua. Wiki iliyopita serikali iliruhusu magari kupita njia tatu wakati wa foleni kali na kuongeza askari wa usalama barabarani. Pia kuna mipango mingine ya muda mrefu, mfano kupanua barabara na kujenga madaraja kwenye makutano ya barabara kubwa. Ninaipongeza serikali kwa juhudi hizi.

Hata hivyo, je dhana ya kupunguza foleni kwa kupanua barabara ni suluhu endelevu? Pengine cha muhimu siyo kupanua njia za barabara, lakini badala yake kupunguza idadi ya magari, hasa ya binafsi, yanayoingia mjini.

Foleni ni tatizo ambalo limeshaikumba miji mingi duniani. Baadhi ya miji hiyo imefanikiwa kupata ufumbuzi wa tatizo hili. Ingefaa kujifunza kutoka kwa hao wenzetu.

Mfano, jiji la London ina utaratibu wa kutoza ushuru magari binafsi yanayoingia katikati ya jiji hilo. Ushuru huo ni Pauni 8 kwa siku. Magari hayo yanatozwa ushuru kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa 12 jioni. Lengo la utaratibu huu lilikuwa ni kupunguza foleni, uharibifu wa mazingira na idadi ya magari yanayoingia mji wa London. Inasemekana utaratibu huu ulipunguza foleni kwa zaidi ya asilimia 20. Nchi nyingine nyingi zimeiga mfumo huu ukiwemo mji wa Melbourne nchini Australia, na miji ya Ujerumani, Norway na Singapore. Kote umeleta mafanikio makubwa.

Jitihada za kutafuta suluhisho la kudumu zilenge katika kuandaa mazingira yanayowavutia watu kutumia usafiri wa umma badala ya magari binafsi, sio kwa kupanua barabara. Lengo kuu liwe kupunguza idadi ya magari yanayoingia mjini. Taratibu zilenge kujenga motisha kwa wananchi, na siyo kuunda lundo la sheria au maagizo. Tunaweza kuleta hali nzuri kwa kuzingatia hoja tatu zifuatazo:

1. Kulipisha ushuru magari (road tolls) binafsi yanayoingia mjini. Serikali inaweza kutoza ushuru sehemu maalumu kuingia mjini. Ada inaweza kuwa sh 2,000/- kwa magari madogo (au 40,000/- kwa mwezi) hadi sh 5,000/- kwa 'mashangingi' (au 100,000/- kwa mwezi). Magari yatalipishwa ada hizi wakati kuanzia saa 12.30 asubuhi mpaka saa 1.30 jioni. Wote, zikiwemo gari za "STJ' na za mabalozi, watakiwe kulipa ushuru.

Utaratibu huu utatunufaisha kwa mengi. Kwanza, utawafanya watu wasipendelee kutumia magari yao binafsi, badala yake watatembea kwa miguu au kupanda daladala. Pili, watapunguza safari za mara kwa mara zisizokuwa na msingi. Tatu, serikali itapata kipato kutokana na ushuru utakaotozwa. Nne, utasaidia kurekebisha mgawanyo wa rasilimali kwa sababu ni matajiri na watu wa kati tu ndio watakaokuwa wanalipa.

Fedha inayotokana na ushuru ziwekwe hadharani kila siku kuwezesha wananchi kufahamu ukweli na kudhibiti rushwa. Fedha hizi zinaweza kutumika kununulia vitabu kwa ajili ya maktaba au kuendesha mabasi maalum ya kusafirisha wanafunzi. Hivyo, hata walipa ushuru watajisikia wanachangia maendeleo ya nchi.

2. Kuboresha usafiri wa umma. Usafiri wa umma unapaswa kuwa mzuri, wa haraka, unaoaminika, safi na gharama nafuu. Lengo ni kuwavutia watu kupanda daladala kuliko magari yao binafsi. Usafiri wa umma unaweza kuboreshwa kwa njia nyingi. Kwanza kwa kupunguza au kuondoa kabisa mabasi madogo (vipanya) mjini na kuongeza mabasi makubwa. Hii inawezekana aidha kwa kuvinyima leseni vipanya au kutoza kodi kubwa kwa vipanya. Hii itawavutia wafanyabiashara wengi kununua mabasi makubwa badala ya madogo.

Pili, kuhakikisha mabasi yanabeba watu idadi iliyoruhusiwa, pia haziishii njiani bila kufika zilikopangiwa kwenda. Tatu, kusisitiza usafi na ubora wa magari yenyewe; magari mabovu kamwe yasiruhusiwe kubeba abiria. Usafiri wa umma ukiboreshwa watu wengi watapenda kuutumia hata maofisaa wakubwa, kama ilivyo kwa nchi za Ulaya ambapo hadi mawaziri wanatumia usafiri wa umma.

3. Kuchochea utumiaji wa vyombo visivyokuwa vya moto. Sasa hivi miundombinu haiwezeshi watu kutumia usafiri kama baiskeli au kutembea kwa miguu. Hivyo hatuna budi kuanza kutilia maanani suala hili. Hii ni pamoja na kutenga njia maalum za waenda kwa miguu na za baiskeli.

Usafiri wa baiskeli au kutembea kwa miguu una faida nyingi. Moja itapunguza foleni. Pili ni nzuri kwa mazingira. Magari yanatoa hewa chafu ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu. Tatu ni nzuri kwa afya zetu (mazoezi). Watu wengi tanafanya kazi wa kukaa siku nzima maofisini, hivyo kutembea kwa miguu au baiskeli itawasaidia kujenga afya za miili yatu na kuepuka magonjwa.

Kuongeza njia za magari sio mkakati wa kudumu. Msisitizo uwekwe katika kupunguza magari binafsi yanayoingia mjini na kuweka mazingira yatakayowafanya watu kupenda kutumia usafiri wa umma na usafiri mbadala kama baiskeli. Changamoto za karne ya 21 zinahitaji fikra pana na endelevu, na viongozi wenye uwezo wa kutuwezesha sisi sote kufikiri mbele zaidi.

Elimu na afya: Upatikanaji kwanza, ubora baadaye?

Na Robert Mihayo
Ilichapishwa 12 Juni 2007

Miongoni mwa maswali aliyoulizwa Rais Jakaya Kikwete alipokutana na wahariri wiki iliyopita lilikuwa ni lini Serikali itaanza kuzingatia ubora wa elimu nchini.

Rais alijibu kuwa kwa sasa Serikali inatilia mkazo zaidi ujenzi wa shule ili kuhakikisha watoto wote wanapata shule (access). Suala la ubora ingawa ni muhimu litafauata.

Huu ndio mtazamo wa viongozi wengi nchini. Mathalani, Rais Mstaafu, Benjamin Mkapa, aliwahi kuuliza: Mzazi gani angekuwa radhi mwanae akose shule eti kwa sababu pesa hazitoshi kujenga shule nyingi zinazotoa elimu bora?

Pengine tunapaswa kujiuliza: Hivi maana halisi ya upatikanaji (access) ni nini? Iwapo nina njaa, kwangu mimi upatikanaji ni pale nitakapoweza kukipata chakula, kukila kwa kukifurahia hadi nitakaposhiba. Iwapo nataka kula pale Hotel Kempinski, kama sina hela za kutosha hakuna upatikanaji. Au nikiwa mbali na ile hoteli na sina usafiri hakuna upatikanaji. Vile vile hata kama mtu ananipeleka Kempinski, kama hoteli haina chakula, vyombo vya kulia au wahudumu, kunipeleka pale hakutanishibisha. Inawezekana kweli nikayashangaa majengo, makochi na hata mandhari yake. Lakini bila kupata chakula siwezi kufurahia kuwapo pale. Ninachohitaji ni chakula, afadhali hata cha yule Mama Lishe wangu wa Tabata.

Hivyo hivyo, kuwa na shule au zahanati, hata kama majengo na madhari yake yatakuwa ya kuvutia namna gani. Bila shule kuwa na walimu wazuri, vitabu na vifaa vingine vinavyohitajika, au zahanati kuwa na wahudumu, vifaa na dawa, upatikanaji wake pekee hauna maana. Upatikanaji sharti uende sambamba na huduma bora.

Kwa mantiki hiyo hiyo, kumwandikisha mtoto katika shule yenye majengo mazuri peke yake hakumusaidii mtoto kuelimika. Anachohitaji yeye ni kupata elimu itakayomwezesha kukabiliana na changamoto za maisha. Hili linahitaji walimu wenye uwezo, moyo wa kufundisha pamoja na vifaa kama vile vitabu, maabara, n.k. Haya ndiyo yanamsaidia mwanafunzi kukuza uwezo wake wa kujifunza; majengo mazuri pekee hayaelimishi!

Hata mgonjwa anapopelekwa hospitali anachokitaka ni daktari atakayemhudumia, vifaa na dawa; si kufurahia uzuri wa majengo ya hospitali! Huduma bora ndiyo itamrudishia afya yake. Afadhali kuhudumiwa chini ya mwembe kuliko kutohudumiwa ndani ya jengo la kisasa!

Mambo matatu yanapaswa kupewa kipaumbele.

Kwanza, mafunzo ya wataalamu wa elimu na afya yaimarishwe na maslahi yao yaboreshwe. Ujenzi wa nguvukazi uzingatiwe zaidi kuliko ujenzi wa majengo.

Pili, kila mwananchi apewe fursa ya kupata angalau huduma ya msingi katika elimu au afya. Shule ziwe na walimu wazuri na wenye moyo wa kufundisha, vifaa vya kufundishia, maabara, vitabu, nk. Pia kila zahanati iwe na wataalamu wa afya, vitendea kazi pamoja na dawa za kinga na kutibu maradhi ya kawaida.

Tatu, kupunguza vikwazo vilivyopo katika upatikanaji wa huduma hizi. Hapa

tunaipongeza Serikali kwa hatua ilizokwishachukua kuhakikisha watoto wengi wanaenda shule. Hatua hizi ni pamoja na kufuta ada za shule za msingi na kuzipunguza kwa shule za sekondari, kudhibiti michango holela na kutoa ruzuku kwa shule zote za msingi za umma chini ya MMEM. Hatua hizi zimewawezesha hata watoto wa maskini kupata nafasi ya kwenda shule.

Badala ya kung'ang'ania kuanza na upatikanaji wa shule ama zahanati na baadaye ubora, Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapewa uwezo wa kupata angalau huduma za msingi. Hili litawezekana iwapo itahakikisha kuwa gharama zake zinakuwa chini na huduma zinatolewa na watu wenye taaluma na nyenzo zinazotakiwa.

Aidha, dhana ya kuanza na majengo na baadaye kuboresha elimu haijathibitishwa kwa vitendo. Tulipoaanza MMEM tuliambiwa kwanza tujenge shule nyingi ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kwamba baadae tungeanza kuboresha elimu. Hili hadi leo halijafanyika ya kutosha.

Hivi karibuni umeanzishwa mpango wa shule za sekondari (MMES). Kweli shule nyingi zimejengwa; lengo likiwa kuwa kila kata iwe na angalau shule moja ya sekondari. Ili kukabiliana ongezeko hili kubwa na la ghafla, Serikali imebuni mpango wa kupata walimu wa chapchap wa kufundisha katika shule hizo. Ahadi bado ni ileile: kwa sasa tuaangalie zaidi access; suala la ubora litafuata baadae. Haitakuwa ajabu kama ahadi hii ya kuboresha elimu itaendelea kutolewa hadi kidato cha tano na hatimaye Chuo Kikuu!

Katika sekta ya afya mambo ni yale yale. Kuna mpango wa kujenga zahanati katika kila kijiji wakati zilizopo nyingi hazina wataalamu wala dawa. Baadhi zimefikia hatua hata ya kufungwa kwa kukosa wataalamu. Kwa mfano, wakati wa ziara yake mkoani Rukwa, Rais Kikwete alisomewa taarifa kuwa mkoa huo una madaktari 7 tu. Aidha, mkoa huo ulikuwa umelazimika kufunga vituo na zahanati 12 kutokana na kukosekana kwa wahudumu wa kuziendesha! Kitaifa kuna upungufu wa 62% ya watumishi katika hospitali za serikali na binafsi.

Sasa katika hali kama hii, kuendelea kujenga shule, vituo vya afya na zahanati itasaidia nini?

Walemavu: Tatizo ni ulemavu au jamii?

Na Gervas Zombwe
Ilichapishwa 31 Julai 2007

Pamoja na kampeni ya kuhamasisha haki za binadamu hasusani haki ya elimu, kwa walemavu wengi Tanzania, haki hii bado ni ndoto.

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) wa mwaka 2005, unabainisha kuwa mwaka 2000 chini ya 1% ya walemavu ndio waliokuwa shule. Aidha, Ripoti ya mapitio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ya mwaka 2006, pia inaonesha kuwa ni 3% tu ya walemavu ndio wako shule. Je, wengine wako wapi?

Kongamano la kimataifa juu ya elimu kwa walemavu lililofanyika 1994 huko Salamanca, Hispania lilitoa tamko la kutoa elimu kwa walemavu wote. Ingawa Tanzania iliridhia Tamko hili na haki za walemavu zinatambuliwa ndani ya katiba, bado taarifa za MKUKUTA na MMEM vinatupa takwimu hizi za kutisha. Ukweli ni kuwa idadi kubwa mno ya walemavu hawako shule. Hebu tujiulize,tatizo hasa ni jamii au walemavu?

Tumezoea kusikia kauli za huruma, msaada, huzuni na kuwajali walemavu. Hata baadhi ya walemavu wenyewe wanadhani hawana uwezo, ni watu wa kuonewa huruma, kusaidiwa, na kufikiriwa. Mtazamo huu unadidimiza haki za walemavu.

Ulemavu ni hali ya sehemu moja ya mwili kuwa dhaifu au haipo. Lakini hali hii haiondoi uwezo wa mlemavu. Pamoja na udhaifu au upungufu huu, walemavu wana uwezo mkubwa wa kufikiri, kutenda, kubuni, kuamua, kujieleza na hata kuthubutu.

Tuna mifano mingi ya walemavu wenye uwezo mkubwa mashuleni na hata sehemu za kazi,wakatui mwingine hata kuzidi watu wasio na ulemavu.

Tunao maprofesa, wahandisi, madaktari, wanasheria, na wanamuziki mahiri wenye ulemavu. Pia wapo wahunzi, wachongaji, wasusi, wafugaji, wakulima, wafanyabiashara na wenye ulemavu. Hivyo, walemavu wanaweza! Tatizo ni jamii inayowanyima fursa.

Udhaifu wa kiungo kimoja hauondoi uwezo wa kiungo kingine. Ulemavu wa mguu haumfanyi mlemavu ashindwe kusikia au kuona.wala ulemavu wa masikio haumfanyi mtu huyo ashindwe kufikiri na kutenda. Je mlemavu asiyeona pia anashindwa kufikiri au kusikia? Au mlemavu wa viungo hawezi kusoma au kuandika?

Mitazamo hasi ya jamii juu ya ulemavu ndiyo kikwazo cha kuheshimu haki za walemavu. Na hii imejikita kwenye maeneo haya:

Kwanza, jamii ina historia ya kuwaacha nyuma walemavu. Historia ya elimu Tanzania inaonesha kipindi cha nyuma hakuna mlemavu aliyapata elimu. Kwa sababu shule na vifaa vyao havikuwepo. Ujenzi wa shule maalumu kwa walemavu umeanza juzijuzi tu. Mathalani, shule maalumu za walemavu wa macho kama Bwigili, Uhuru na Tabora zilianza miaka ya 1964 na miaka ya 1980.

Aidha, shule za walemavu wa masikio kama vile Buguruni na Tabora zilijengwa mwaka 1974 na 1982. Kabla ya hapo shule maalum za aina hii hazikuwepo; lakini hata zilipojengwa bado ni chache zikilinganisha na mahitaji. Shule za walemavu wa Akili kama vile zilizopo Sinza na Mtoni nazo zimeanza hivi karibuni tu hapa Dar es Salaam na sehemu chache mikoani. Walemavu wengine wanasomea wapi?

Pili, kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa viongozi wetu pia ni tatizo. Viongozi wanatunga sera zinazowabagua walemavu. Mfano mzuri, ni Sera za Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari.

Ingawa sasa hivi kuna ongezeko kubwa la majengo ya shule za msingi na sekondari, lakini majengo maalum kwa walemavu hayapo. Hapa tena inatupasa tujiulize, je, tatizo ni walemavu au watunga sera?

Tatu, kukosekana kwa mahitaji ya walemavu pia ni kikwazo. Mathalani, wanafunzi walemavu wa macho wanahitaji mashine maalumu za kuandikia na fimbo za kutembelea. Lakini wengi hawana. Aidha, majengo yasiyo hata na sehemu ya kupita walemavu yanajengwa kwa mabilioni ya fedha huku vifaa vya walemavu hakuna. Hii ni haki?

Nne, ndani ya jamii pia kuna matatizo. Takribani nyumba na ofisi zote za umma hazina njia za walemavu. Hata baadhi ya makanisa na misikiti wanakohubiri upendo hakuna njia za kupitisha baiskeli za walemavu. Je haya ni sawa?

Tano, ingawa waajiri katika makampuni binafsi na idara za serikali wanatangaza nafasi za kazi, wakati mwingine hata kwenye sekta ya walemavu, hawawapi kipaumbele walemavu. Aghalabu, tuona "mabosi" wengi wa miradi ya walemavu ni watu wasio na ulemavu. Kwa nini nafasi hizo wasiachiwe walemavu wenyewe?

Ulemavu ni hali ya udhaifu na kila mtu anaweza kuwa nayo kwa namna moja au nyingine. Fikiria profesa wa Kiswahili akienda China. Je, ataweza kuongea kichina au atakuwa kimya? Je tunapaswa kumwita bubu au dhaifu kwa sababu hawezi kuongea kichina? Vivyo hivyo, fundi ujenzi akipewa mti achonge kinyago ataweza? Na iwapo atashindwa ni haki kumuonakuwa ni mtu dhaifu wa kuonewa huruma?

Ni ajabu na siyo haki kuwatambua watu wenye ulemavu kama watu wasiojiweza na hivyo wanaohitaji kuhurumiwa, kusaidiwa, na kuhuzunikiwa. Kutambua uwezo wao na kuwapa haki zao hasa elimu na fursa ndio jambo la muhimu. Kuwanyima fursa walemavu ni kudidimiza maendeleo ya nchi.

Wahenga walisema, jambo usilolijua ni sawa na usiku wa giza! Hili ni dhahiri kwa jamii kubwa ya watanzania, hasa waishio maeneo ya vijijini. Sera nyingi na mipango ya program za maendeleo kwa kiasi fulani bado ni usiku wa giza kwao. Hili linawafanya washindwe kushiriki katika maamuzi, kutoa maoni na hata kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango hiyo kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla. Changamoto hii inafanya suala la upatikanaji habari, utafiti, elimu na kuibua mijadala katika jamii kuwa la lazima.

Safu ya *Kauli Mbadala* katika gazeti la *Mwananchi* kila Jumanne, pamoja na *Hard Questions* kila Jumatatu katika gazeti la *The Citizen* zimebuniwa kwa lengo la kukabili changamoto hii. Waandishi toka ndani na nje ya HakiElimu, wakitumia tafiti, wanahabarisha umma. Maeneo muhimu yanayogusiwa ni elimu, utawala, haki za binadamu, afya na demokrasia. Kupitia safu hii ya maoni, tunatarajia jamii ihabarike, ielimike na ipate ari ya kuibua mijadala makini yenye lengo la kuleta mabadiliko katika jamii. Pengine mabadiliko haya ndio maendeleo tunayoyahitaji hapa nchini.

Kitabu hiki ni mkusanyo wa *Kauli Mbadala* 29 zilizoandikwa na waandishi 13 tofauti na kuchapishwa na gazeti la Mwananchi mwaka 2006 na 2007. Tunataraji maoni yatawagusa wasomaji na pengine kuchukua hatua za kivitendo inapobidi.

Kwa mawazo, hisia, maswali na mchango wa maoni tutumie kwa barua pepe, paa@hakielimu.org

hakielimu

Mwananchi Communications Ltd